*République Démocratique du Congo*

**MINISTERE DE L'ENVIRONNEMENT, CONSERVATION DE LA NATURE ET TOURISME**

---------------------------------------------

**Institut Congolais pour la Conservation de la Nature (ICCN)**



# Kitabu Cha Haki Na Sharti Za Shirika Ndani Ya Eneo Zenye Kukingwa

*Mwezi wa tatu 2011*

## DAFTARI

KITANGULIZI ........ 3

I. MAINGILIO ........ 4

II. MAMBO KWA JUMLA JUU YA ENEO ZINAZO KINGWA ........ 5

II.1. Aina Za Eneo Ya Kukingwa ........ 5

II.1.1. Akiba maumbile nzima ........ 6

II.1.2. Hifadhi ya taifa ........ 7

II.1.3. Akiba ya yote yenye maisha katika eneo ........ 8

II.1.4. Akiba ya misitu ........ 9

II.1.5. Akiba za nyama na za yote yanayo husu mawindo ........ 10

II.1.6. Sehemu zenye kukingwa ........ 12

II.2. Umbo Kisheria Ya Eneo Zenye Kikungwa ........ 13

II.3. Kuundwa Kwa Eneo Zenye Kukingwa ........ 13

II.4. Misitu Za Kupangwa Zilizo Undwa Na Sheria Ya Waziri, Amri Ya 15 Sheria Ya Msitu ........ 15

II.5. Siasa Ya Mazingira Ya 15/100 Ya Eneo Lote La Udongo Ya Inchi Inayo Semwa Katika Amri Ya 14 Ya Buku La Sheria Ya Msitu Ina Maana Gani? ........ 17

II.6. Fasi Ya Shirika La Wakaaji Mahali Katika Buku La Sheria Ya Msitu ........ 18

II.6.1. Mwanzo wa jina «wakaaji mahali» katika sharia ya wa kongomani ........ 18

II.6.2. Haki za matumizi ndani ya misitu zenye kupangwa ........ 22

II.7. Muhimu Wa Sheria Na Wa Vyumba Vya Mamlaka ........ 22

II.7.1. Chumba cha sheria ........ 23

II.7.2. Msingi unao husu vyumba vya madaraka ........ 27

III. KIFUPI CHA HAKI NA SHARTI YA SHIRIKA ZINAZO ELEKEA: SERIKALI, CHUMBA CHA KONGO KINACHO HUSIKA NA KUCHUNGA AKIBA LA UMBO AO WATUMISHI WENGINE, WAKAAJI NA SHIRIKA MAHALI ........ 33

III.1. Kibao 1 Akiba Maumbile Nzima: Sheria Ya Raisi 69-041 Ya Agosti 22 1969 ........ 33

III.2. Kibao 2 Akiba Ya Mawindo: Sheria 82-002 Ya Mei 22 1982 ........ 34

III.3. Kibao 3 : Haki Na Sharti Ya Serikali Na Ya Wakaaji Mbele Ya Matumizi Ya Eneo Ya Kukingwa ........ 35

III.3.1. Serikali (mwenye) amri ya manufaa-eneo la kukingwa ........ 35

III.3.2. Chumba cha Kongo juu ya kuchunga akiba ya umbo ao watumishi wengine ........ 37

III.3.3. Wakaaji na vikundi vya wakaaji wa nafasi ........ 37

IV. KWA KIFUPI ........ 40

V. VITABU VILIVYO TUMIWA ........ 41

V.I. Nyaraka Za Serikali (Zinazo Julikana) ........ 41

V.2. Mapatano Ya Mataifa ........ 41

V.3. Vitabu Ao Maandiko Mbalimbali ........ 42

## KITANGULIZI

Umoja wa ulimwengu juu ya akiba ya umbo, yenye kujulikana kwa ufupi UICN, ni offisi ya kwanza ya kutenganisha eneo za zikipangwa kufuatana na shaba na sharti fulani.

Ndani ya kitabu hiki, kuona kama kila eneo ya kukingwa ina shaba ya upekee, ni ya muhimu kujulisha kwa wote, yenye kukatazwa na yenyi ina ruhusiwa. Ndani ya aina zote za eneo za kukingwa.

Inafaa kujuwa kama kila inchi, kufwatana na faida ya mazingira yake, ina unda eneo za kukingwa na inatia namna ya kuyaongoza na shaba ya matumikishi.

Hii buku iliandikwa na mwalimu Kalambay Lumpungu wa Darasa la sheria ya masomo ma kuu ya Kinshasa, kwa shabaa ya kuonesha kwa somo la kwanza kwa vikundi ndani ya eneo zilizo kingwa. Ili oneshwa na kuhakikishwa na kamati ndongo iliyo undwa chini ya uongozi wa chumba cha hasabu na matengazo ya pori (DIAF) ya chumba cha waziri wa mazingira akiba na Matembezi.

## KIFUPI CHA MATUMIZI

Kitabu hiki kina vipande viwili.

Kipande cha kwanza kina nucta ifatayo: akiba za pori, eneo za kukingwa na namna ya kuundwa kwake kisheria na muhimu wa sheria na wa vyumba vya kazi ni kusema naraka ya kisheria ilio yaunda na ma offisi inayo husika na matumikishi.

Kipande cha pili kina kifupi kinacho fanyika kama kibao kufwatana na haki na sharti za serikali, na offisi ya Kongo inayo husika na akiba na mwengine mtumikishaji, na wakaaji na shirika za wakaaji wa nafasi.

# I. MAINGILIO

Kitabu hiki kinasema juu ya eneo inayokingwa na kwa upekee kabisa juu ya pori zinazo pangwa.

Pori zinazo pangwa inaelekea amri ya 12 mpaka 19, 38 na 39 ya sheria ya Raisi 11-2002 ya 29 Agosti juu ya kitabu cha sheria ya pori na sheria namba 08-08 ya Aprili 2008 inayo weka mwenendo wa kupangwa na kuondoshwa kwa pori.

Akiba nzima ilifanyiziwa na sheria ya Raisi ya tarahe 22 Agosti 1969 na akiba ya nyama, katika sheria ya Raisi 82-002 tarehe 28 Mei 1982 na mipango ya kuyatumikia.

Pori ya kupangwa iko chini ya mamlaka ya Waziri mwenye kuhusika na pori, na kwa siku hizi, na Waziri wa mazingira, akiba za maumbile na matembezi. Akiba nzima na akiba ya nyama inapewa kwa chumba cha Kongo kinacho husika na akiba ya umbo kama vile kiongozi.

Kufwatana na mapangilio ya sheria, pori za kupangwa, akiba nzima na akiba ya nyama inapatikana ndani ya mali muhuri wa serikali. Inaitwa mali muhuri, vitu vyenye vinawezwa hamishwa, vyenye haviwezi hamishwa ao udongo unao kuwa wa serikali ao kwa offisi muhuri kama vile chumba cha Kongo kinacho husika na akiba ya umbo, na zenye haziwezi kupewa mtu binafsi kwa sababu ya umbo zao ao kwa shabaa zilizo pewa. Ndio maana mipango yote yenye kuyatumikisha ni ya muhuri na kuto kuheshimu mipango hiyo inapashwa kufafanushwa sana.

Ndani ya kitabu hiki, yanaitwa vikundi vipatikanamo, serikali, ma offisi zinazo husika na eneo za kukingwa, wakaaji wa kandokando ya eneo inayo kingwa na mashirika zisizo za serikali zinazo ruhusiwa na serikali na inayo tumika kazi zinazo julikana na kupatikana ndani ya kanuni zao, kazi hizi zinaangalia mazingira kwa jumla na pori kwa upekee, amri ya 32, sheria ya msitu (Code forestier).

Kitabu hiki kinagawanywa kwa vipande viwili: cha kwanza kinasema juu ya maneno kwa jumla kufuatana na vyumba ao ma offisi ya matumizi na cha pili kinafanya kwa kifupi kwanza kazi zinazo katazwa ndani za eneo za kukingwa na ruhusa inayo panwa na pia haki na sharti ya serikali, ya offisi ya Kongo inayo husika na akiba za umbo ao mwengine mtumikishaji na wakaaji mbele ya matumizi ya pori za kupangwa na eneo za kupangwa.

# II.MAMBO KWA JUMLA JUU YA ENEO ZINAZO KINGWA

Chini ya nukta hii; kutasemwa kwa kufatana juu ya eneo za kukingwa na kwa upekee juu ya pori ya kupangwa.

## *II.1. Aina Za Eneo Ya Kukingwa*

Umoja wa ulimwengu juu ya akiba ya umbo, yenye kujulikana kwa ufupi UICN, ili hesabu na kupanga eneo za kukingwa kutokana na kibao cha aina, shabaa na sharti. Kwa mwaka 1974, utenganisho ulionyesha tu aina ine[1]. Kwa mwaka 1978, aina kumi zilitenganishwa na kuhesabiwa[2]. Kwa mwaka 1992 hesabu ilitoka kumi na ilishuka aina tano za eneo ya kukingwa[3] na katika 1994, ndani ya kupangwa kwa eneo zinazo kingwa na UICN kuna hesabiwa aina saba[4]. Kutenganishwa huko kwa sasa kunaenda tokea daraja ya matumizi ya watu kidogo kufikia utendaji wa watu wengi na ambao shabaa halali ni kuleta namna ya kulinganisha kati ya mataifa. Aina hizo ni:

1. Aina I a: Akiba ya maumbile nzima;
2. Aina I b: Akiba ya maumbile ya pori;
3. Aina II: Hifadhi ya taifa;
4. Aina III: Jumba maumbile;
5. Aina IV: Eneo inayo tumikishwa kwa makao aina zingine zinazo maisha;
6. Aina V: Hali ya inchi ao ya maji ya kukingwa;
7. Aina VI: Eneo za kukingwa ya manufaa maumbile yenye kutumikishwa.

Aina saba zipatikazo toka nucta I na mpaka VI ina onekana sawa eneo maumbile ya kukingwa. Namba yenye ina patiliwa kwa kila aina hai onyeshe kama ni ya muhimu kupita ingine lakini inaenda toka daraja ya utumizi udogo mpaka utumizi wa watu wengi katika matumikishi; aina zote zinazo kuwa na UICN ni za muhimu na zina saidiana kwa kuchunga akiba kwa mahali ya mambile[5].

---

[1] Trinto Mugangu, namna za uhakimu na aina za eneo za kukingwa, 2008, ukurasa wa 1.

[2] Stéphane Doumbé-Billé, Haki ya mataifa kwa ajili ya eneo zinazo kingwa, katika eneo zinazo linganishwa, matendo tarehe ya pili ya DA-mafunzo ya mazingira, Tunis, 2001, ukurasa wa 16.

[3] Mamoja na nukta ya 2.

[4] Trinto Mugangu, Op cit, ukurasa wa 1.

[5] Trinto Mugangu, Op cit, ukurasa wa 1.

Eneo za kukingwa ni neno kubwa inayo patikana ndani ya sheria ya mazingira. Msemwa «eneo ya kukingwa» si jina ya uhakiki. Juu ya yote, ina wezakana kwa kusomwa vyombo vya mapatano, kwamba ni jina lenye kutumikishwa, yenye haiwezi kusimama mbele ya majina mengine yenyi inasaidia kutaja ile ile mbinu ya uchungaji, lakini yenye kwa wakati ule ule, inapewa maana yenye kuwa umbali mbali, kufwatana na shaba ya uchungaji ulio tafuti [6].

Ndani ya mapatano mengi, mnapatikana masemi «Kata ya kuchungwa», lakini matumizi ya masemi «eneo za kuchungwa» ina neema kwa mafundisho na inatumiwa sasa ndani ya vyombo vimoja vipya vya uchungaji.

Ina onekana kutokea sheria ya kufananishwa kama umbali mbali wa eneo za kukingwa ni kewli[7]. Kwa kweli kuna eneo nyingi za kukingwa kama vile pia aina za ukingo unao tafutiwa.

Kwa yenye kwangalia Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo, kunapatikana vitenganisho sita vya eneo ya kukingwa.

### II.1.1. Akiba maumbile nzima

Akiba maumbile nzima ni eneo ya kukingwa, yenye kuwa chini ya uhakimu, sababu zaidi ya mafunzo ya utaalamu, iko eneo ya udongo, ya maji, ipatikamo yoyote yanayo maisha katika ulimwengu, yote ya madini ao umbo yoyote inayo onekana sawa sanamu ao miandiko ao tena aina yote inayo onekana ao kuonyesha, inayo akimishwa hasa zaidi kwa ajili ya utaalamu na ukingo unao endelea wa mazingira.

Shabaa za matumizi kwa aina I.a ni ya:

- Kuchunga (biotopes) ya yote inayo maisha ya aina ndani ya sharti maumbile ao zinazo badilishwa;
- Kusimamisha himara manufaa ya vizazi katika hali ya kuyaendesha mbele;
- Kusimamisha imara mtindo wa maisha yote inayo patikana;
- Kuchunga vizuri yote inayo patikana ndani ya mipangilio ya hali ya nafasi ao mjengo ya mawe;

---

[6] Stéphane Doumbé Billé, Op cit, ukurasa 15.

[7] Mishel Prieur, Eneo za kukingwa katika sheria ya Ufaransa ukurasa 38-50; Gerd Winter, eneo maumbile zinazo kingwa za bahari na za ardhini, ukurusa 84-92; Op cit.

- Kuchunga mahali maumbile yanayo kuwa mifano mizuri kwa ajili ya mafunzo ya utaalamu, kwa uchungaji unao endelea wa mazingira na kwa maadibisho pia eneo mifano, wakiondoshwa njia zote zinazo wezekana kuepushwa;
- Kupunguza hata kidogo misukosuko, ikipangwa na kufanya na angalisho kazi zinazo ruhusiwa, mafunzo na mambo mengine yote.
- Kutia mipaka kwa kupitia watu wote[8].

Akiba maumbile mzima yanayo semwa ndani ya sheria ya Raisi 69-041 ya Agosti 22 1969 na ina undwa na sheria ya Raisi wa Jamhuri, amri ya 1.

### II.1.2. Hifadhi ya taifa

Hifadhi ya taifa, ni eneo la kukingwa, linalo kuwa chini ya uhakimu kwa lazima kuu, la kuchunga yote yanayo kuwa maisha ndani ya msitu huu na kwa sababu ya kuyaunda upia[9].

Muundo wa hifadhi ya taifa ndani ya mtaa inawezekana, wakati akiba ya nyama, pori, udongo, chini ya udongo, maji na kwa jumla, mahali maumbile yanayo onesha faida muhimu na inayo lazimishwa mahali haya yachungwe.

Shabaa ya matumizi ya hifadhi ya taifa ni hii ifuatayo:

- Kukinga eneo maumbile na hali ya muhimu ya taifa na mataifa juu ya matumizi ya shabaa ya utaalamu, maadibisho ya kiroho, ya michezo ao matembezi;

- Kuendelesha, kufuatana na sharti maumbile yanayo wezekana, mifano inayo onyesha eneo ya kuchafuka, vikundi mbalimbali vya yote ya maisha, ya manufaa ya vizazi na ya aina, iki hakikisha ustawi na umbalimbali wa yote yanayo kuwa na maisha;

- Kutia mipaka na kwa wakati ujao, kuepusha mbele ya wakati namna yote ya matumizi ao ya kukaa kusio patana na shabaa ya kanuni ya kuweka akiba; kulazimisha heshima ya yote ipatikanayo ndani ya maisha ya mahali, hali maumbile inayo wekwa pembeni ao ya kupendeza inayo hakikisha kanuni ya hifadhi ya taifa;

[8] Trinto Mugangu, Op cit, ukurusa 1-2
[9] Mamoja na nukta 8, ukurusa 2

- Kujua lazima ya wakaaji wa asili pia matumizi ya manufaa kwa shabaa ya maisha yao ikionekana kama yote haya hayataleta tatizo kwa shabaa zingine za matumizi.[10]

Mtaa unao wekwa kuwa msitu wa taifa juu ya kufuga, unapashwa kuendelezwa kwa hali yake maumbile, milima na mabonde ya lazima inayo weza kuonekana, ukingo wa yote inayo maisha ya manufaa ya vizazi na aina zinazo kuwa ndani ya hatari ya kumalizika, kwa ajili ya kuchunga ustawi na umbali mbali wa yote inayo maisha katika eneo ya pori.

Hifadhi ya taifa unatumikishwa na chumba cha wa Kongomani kinacho husika na akiba ya umbo, ikijulikana kwa jina la «Akiba Maumbile Nzima». Kwa hiyo inafaidika na kuchungwa na ukingo mzima na kuchungwa kunakofaa ao pamoja na kukatazwa kwa kazi zote za watu zisizo ruhusiwa na sheria.

Kwa yote yanayo angalia akiba maumbile na hifadhi ya taifa katika masemi yaliyo semwa kwa kufunguliwa mkutano juu ya mazingira ya N'sele Septemba 9 1975 – ambayo msingi ulikuwa «akiba la umbo na mamlaka ya kukamata mipango». Raisi Mobutu alisema: «Katika muda wa miaka kumi (10) tume unda misitu za ukingo na za akiba maumbile kupita yalio undwa na walio tutawala muda wa miaka makumi ma nane. Na shabaa letu ni kufikia kwa asilimia kumi na tano juu ya mia moja (15%) ya inchi nzima inayo weza kuhakikishwa tukiangalia ukubwa wa Zaïre (Jamhuri ya Kidemocratia ya Kongo), ukubwa zaidi ya Ujerumani zote mbili.»[11] Hifadhi ya taifa inaundwa kwa njia ya sheria makamu ya Raisi wa Jamhuri.

Hifadhi ya taifa zinajulikana kuwa inne (4): Mali ya dunia nzima kupitia UNESCO: hifadhi ya taifa ya Virunga - 800.000 Ha; hifahi ya taifa ya Garamba - 500.000 Ha; hifadi ya taifa ya Kauzi-Biega - 600.000 Ha na hifadhi ya taifa ya Salonga - 3.600 Ha.

### II.1.3. Akiba ya yote yenye maisha katika eneo

Shabaa kubwa ya akiba ya yote inayo maisha ni kuweka akiba kwa lazima ya leo na ya kesho, kwa kuonesha umbalimbali na lazima ya yote yanayo maisha mahali fulani na kuchunga umbalimbali wa vizazi via aina vilivyomo kwa maendeleo.

Imewekwa kufuatana na usikivu wa UNESCO kila akiba inakuwa na eneo makutano ya ukingo mzima, moja ao sehemu nyingi ya kupitia, moja ao sehemu

---

[10] Trinto Mugangu, Op cit, ukurasa 1-2.
[11] Mobutu, masemi, usomi na habari, 1965-1975, kitabu cha II, ukurasa 619.

nyingi ya kupimia. Uanzisho, sehemu ya matengenezo ya namna ya kutoa mazao, sehemu ya kuharibika zinazo chumgwa na eneo la mapitio [(12).]

Akiba ya maisha ya ndani ya eneo linapashwa kuleta njia ao kusaidia kwa utaalamu wa maisha kufuatana mahali yao, ya muhimu na ya kutumikishwa mara moja mahali kawaida na mahali panapo kuwa maji.

Faida ya eneo hizi ni ya kutoa msimgi wa mifano inayo ruhusu kujua mabadiliko kwa muda mrefu kwa yote yanayo angalia maisha katika eneo; ni ya lazima saana kwa ukingo unao endelea wa mazingira.

Akiba ya yote inayo maisha katika eneo yana timiza kazi ine:

1. Kazi ya akiba kwa namna ya ufunguzi;
2. Kazi ya utaalamu na ya kuchunga kunako endelea;
3. Kazi ya kufunza na kufundisha;
4. Kazi ya kutumika pamoja kwa maendeleo.[13]

Akiba ya yote yanayo maisha katika eneo linalo tumikishwa katika chumba cha Waziri anae angalia mazingira, kupitia chumba cha akiba ya umbo. Ni lazima kujua kwamba hakuna nyaraka inayo ongoza ndani ya Kongo mambo yanayo angalia akiba ya yote yanayo maisha katika eneo.

### II.1.4. Akiba ya misitu

Mpango wa taifa wa kutumikisha mazingira (PNAE), ndani ya «hali ya sasa ya mazingira katika Zaïre» ya Septemba 1996 inataja kati ya eneo zinazo kingwa akiba ya misitu[14].

Akiba ya misitu zina shaba ya: Ukingo wa misitu maumbile, maendeleo ya utaalamu wa yote yanayo angalia misitu, ustawisho wa misitu maumbile kwa ajili ya kuendelesha, kutoa mazao ya miti ya kuchonga sanamu na kuni.

Nyingi za akiba za misitu yameachwa na yanayo baki yametumikishwa vibaya na watu.

---

[12] Matuka Kabala, vyombo vya matumikisho kwa ajili ya mazingira ya 2000-kazi ya UNESCO-akiba ya yote yanayo maisha ndani ya eneo na mali ya dunia, ndani ya matendo ya seminari-mazingira na ustawisho unao dumu, Brazaville tarehe 05-08 Julai 1989, ukurasa 62-63.
[13] Matuka Kabala, Op cit, ukurasa 65-67.
[14] Chumba cha Waziri kinacho angalia mazingira, hifadhi ya umbo na matembezi, mipango ya taifa juu ya kazi ya mazingira (PNAE) hali ya sasa ya mazingira katika Zaïre, 1996, ukurasa 127.

Chumba cha matumizi cha akiba hizi ni chumba cha matumizi ya misitu katika chumba cha Waziri anae angalia msitu (chumba cha kutayarisha na kupandwa kwa miti).

### II.1.5. Akiba za nyama na za yote yanayo husu mawindo

Sheria la bunge la tarehe makumi tatu na moja (31) ya Aprili 1940 linasema: «Kiongozi mkuu na viongozi wa jimbo wanaweza ya kwanza kwa njia ya sheria makamu, ya pili kwa njia ya sheria ya Waziri, kuweka sehemu ya msitu akiba ya mawindo yote ao kwa sehemu kufuatana na namna itakayo inakatazwa kuwinda nyama zote ao aina fulani ya nyama. Ikiwa kwa namna ya sehemu ya misitu ya mawindo iliowekwa akiba ambayo mawindo haya ruhusiwi, isivyo kwa mipango fulani na kwa malipo ya kodi inayo pangwa na sheria makamu ao sheria ya Waziri.»

Katika sehemu ya misitu ya mawindo zilizo wekwa akiba, mawindo yameruhusiwa kwa wakaaji wapatikanamo kwa ajili ya maisha yao.

Sheria 82-002 tarehe 28 Mei 1982 juu ya mawindo imesimamisha vipindi viwili vya «akiba ya nyama». Akiba zote na akiba sehemu. Ya kwanza inahitajiwa kwa ukingo moja na iko ya sehemu aina ya akiba maumbile na ya pili inahitajika kwa ukingo wa nyama kwa ajili ya matumizi yake na yana fanana na sehemu ya misitu ya mawindo. Mafasirio hayo ya mehakikishwa na amri ya 17[15].

Kufuatana na kipengele cha kwanza akiba zote za nyama ni «eneo inayo wekwa pembeni kwa ajili ya akiba, matengenezo na kuendelesha maisha ya nyama ya misitu pia kwa ukingo na ujenzi wa makao ambayo mawindo, uchinjo ao kukamatwa kwa nyama kumekatazwa, isipokua tu kwa viongozi wa akiba ao chini ya ulinzi wao na ambamo majengo na kazi mbalimbali za watu zimekatazwa».

Kufuatana na amri hii moja, hifadhi sehemu ni eneo linalo wekwa pembeni ambamo mawindo yamekanunishwa na kuchungwa kwa namna ya upekee; mipaka zinaweza kutiwa katika muda na namna ya matumikisho na pia namna ya wanyama wanao weza kutumikishwa, matumikisho ya eneo hizi yatatiwa chini ya kanuni ya mpango mmoja unao leta ruhusa ya uhakimu kibarua kia kuruhusu na kodi itahakikishwa na chumba kinacho husika na mawindo.

Kwa hayo, tazama yanayo somwa katika amri ifuatavyo:

[15] Ch. Du Saussay na P. Wilkinson, akiba ya umbo ya Zaïre, mafunzo yote yanayo maisha katika msitu na mpango, ripoti ya mwanzo, ukurasa 13.

- Amri ya 13:

«Ndani ya akiba ya wanyama imekatazwa, isipokua ruhusa ya kiongozi wa nafasi:

1. Kuingiza nyama ya kufuga ao zinazo ingia zenyewe, silaha za moto, mitego ao chombo chote cha mawindo, kuwa nacho, kubeba nyama zote za maisha, ngozi zao ao pembe, minofu yao ao manufaa zingine zote za wanyama;
2. Kufuatana, kuwinda, kukamata, kuogopesha ao kuleta woga kwa namna zote, aina zote za wanyama wa msitu, hata nyama zinazo tapwa na hatari ao kwa wakati wote mgumu.»

«Kwa haya ya mwisho, ikiwa nyama ame umizwa ao kuuwawa, aliye fanya tendo hilo anapashwa kuyajulisha kwa Waziri anae husika na mawindo katika kazi zake ao kwa mjumbe wake alie karibu ndani ya muda wa masaa 48.»

«Anapashwa pia kujulisha kwamba alijikuta katika hatari na ya kuwa hakuchokoza mwenyewe ao kupitia jambo fulani hatari ambayo amejiona kuwa chambo.»

«Akikosa ushahidi ao maelezo yanayo mupa sheria anastahili hukumu unao pangwa katika sheria hii.

3. Kuharibu ao kasambaza kwa namna ilio inje ya kanuni makao ya wanyama wa msitu;
4. Kutumikisha gari la mabawa kwa kipengele kilicho chini ya mita 500.»

- Amri ya 14:

«Ndani ya akiba zote ao nusu za nyama za misitu, kazi zote mbalimbali za watu zilizo kuwa kabla ya kuingizwa kwa sheria hii imekatazwa kama vile:

1. Kuhamisha miji na vijiji;
2. Kuhama kwa wakaaji na maundo ya vijiji vipya;
3. Kulimwa kwa mahali palipo pandwa miti na kwa namna inayo angalia yote, kufanya kazi zinazo weza kuleta hatari kwa ukimya, maendeleo ao matimikisho ya nyama wa misitu.»

- Amri ya 15:

«Waziri anae husika na mawindo katika kazi yake anaweza kuondoa vizuizi vinavyo tajwa katika kitengo kilicho tangulia kwa faida ya vijiji anavyo vitaja na kupitia kanuni anazo zitaja kama vile:

1. Wakati wa matengenezo kupitia sheria zinazo kamatwa makao ya wanyama wa msitu;

2. Wakati wa kusaidia matumizi ya wanyama wa msitu.»

Sehemu ya msitu wa mawindo zipo chini ya ulinzi wa chumba cha wa Kongomani kinacho angalia akiba ya umbo.

### II.1.6. Sehemu zenye kukingwa

Sehemu zote za ardhi ya inchi zisizo chini ya mpango wa kufanywa mji mkuu inaweza kufanywa sehemu ya kuchungwa, kuwa historia, mapambo ao umbo la kutafsiri akiba, kurudishwa upya na kujengwa ao kupewa bei kwa yote ao sehemu ya jumla ya yote isiyoweza kuhamishwa.

Sheria N° 75-024 ya tarehe 22 Julai 1975 inayo angalia sehemu ya kuchungwa inatoa chombo pekee cha kuambatana juu ya ukingo wa umbo kwa ujumla na ya wanyama kwa upekee: ya akiba ao kurudishwa upya ao kujengwa. Sehemu zinazo chungwa zimeundwa kwa njia ya sheria makamu inayo chagua kazi za uhakimu ao shirika linalo husika na matumikisho.

Kipengele cha 2 kina hakikisha kwamba sheria makamu inaweza kuipangia mpango wa upekee na kwa namna nyingine kukataza ndani ya sehemu ya msitu kwa mawindo na kwa uvuvi, kazi za kutumia viwanda, uchuluzi, mlimo, ufugaji ao utumikishaji wa msitu, kuruhusu kazi za watu wote, kuondoa vifaa vya eneo ya kupanwa ao hapana, kutumikisha maji, kutembea huru kwa watu ijapokuwa namna zote wanazo zitumia, kazi zote zinazoweza kuleta magumu kwa maendeleo maumbile ya wanyama na ya msitu na zaidi kwa jumla, ya kutoa maji hali ya sehemu.

Wale wanao fukuzwa kwa ajili ya kuunda sehemu inayo chungwa wanapashwa kulipwa. Kwa hiyo kipengele cha 4 kinasema: «Mabishano yanayo angalia malipo fulani kwa wale wanao tajwa yatatimizwa kwa namna moja na kuondoshwa kwa ajili ya faida ya watu wote. Malipo yatatolewa na serikali».

Tunaweza kuongeza kwa eneo hizo za kukingwa shamba la wanyama na za miti zilizo akiba za inje ya mahali iliyo chakuliwa ya wanyama na ya pori. Inatumikishwa na chumba cha wa Kongomani kinacho husika na akiba ya umbo.

### II.2. Umbo Kisheria Ya Eneo Zenye Kikungwa

Eneo zinazo kingwa za hesabiwa kati ya sehemu ya watu wote walio chini ya ulinzi wa serikali.

Kwa yale yanayo angalia sehemu la eneo la watu wote walio chini ya ulinzi wa serikali, amri ya 55 cha sheria n° 73-021 ya tarehe 20 Julai 1973 inayosema juu ya matumikisho kwa jumla ya vitu, namna ya matumikisho ya msitu na ya vyote visivyo hamishwa na namna ya matumikisho ya uhakika inasema:

«Sehemu za pori ya serikali ni mchango za udongo uliotiwa kwa matumivu ya watu wote.

«Udongo huo hauwezi panwa kwa matumizi kabla haujatiwa inavyo stahili.

«Sehemu ya msitu yalio kwa watu wote na ulio chini ya mamlaka ya serikali zinatumikishwa na mipango ya upekee ya vitu vilivyo wekwa kwa matumizi ao kwa kazi ya watu wote».

Kila moja za eneo zinazo kingwa yana onyesha kwa yale yanayo angalia sheria, kazi zote za ndani ya sehemu zinazo kingwa:

- Yale yalio katazwa kwa jumla;
- Yale yaliyo chini na kuruhusiwa;
- Yale yanayo jibu kwa mipango ya utumwa.

### II.3. Kuundwa Kwa Eneo Zenye Kukingwa

Hifadhi za taifa zime undwa:

- Hifadhi ya taifa ya Virunga, sheria ya tarehe 21 Aprili 1925;
- Hifadhi ya taifa ya Garamba, sheria ya tarehe 17 Machi 1939;
- Hifadhi ya taifa ya Upemba, sheria ya tarehe 15 Mei 1939;
- Hifadhi ya taifa ya Kahuzi-biega, sheria makamu ya tarehe 30 Machi 1970;
- Hifadhi ya taifa ya Salonga, sheria makamu ya tarehe 30 Machi 1970;
- Hifadhi ya taifa ya Kundelungu, sheria makamu ya tarehe 30 Novemba 1970;

- Hifadhi ya taifa ya Kahuzi-biega, sheria ya tarehe 30 Machi 1970;
- Hifadhi ya taifa ya Maiko, sheria makamu ya tarehe 30 Novemba 1970.

Kwa kuunda hifadhi ya taifa, serikali inatumia namna ya kuondosha msitu chini ya mamlaka ya wakaaji kwa ajili ya matumizi ya faida ya watu wote.

Akiba ya yote yanayo maisha ndani ya msitu yameundwa:

- Akiba ya Yangambi katika jimbo la asubuhi kwa mwaka wa 1970;
- Akiba ya Lufira katika jimbo la Katanga kwa mwaka wa 1979;
- Akiba ya Luki katika jimbo la Bas-Kongo kwa mwaka 1979.

Mbele ya sheria ya tarehe 24 Julai 1956, haki za misitu za mazoezo kwa wakaaji wa asili juu ya udongo, zilikua bado kunyanganywa na haki ya kurudilia uwenyeji wa msitu na serikali. Kwa ajili ya matumizi ao faida ya watu wote, kwa yote mbele ya kuondoka katika udongo wao, wakaaji walipashwa kulipwa. Hivyo, tuna soma katika sheria ya tarehe 26 Novemba 1934 inayo angalia kuundwa kwa chumba kinacho husika na hifadhi za taifa, ya fuatayo:

- Amri ya 4:

«Zimeondoshwa ndani za mitaa zinazo tiwa macho kwa amri ya mbele:

1. Udongo wa makao ya wakaaji wa asili;
2. Udongo uliopanwa ao uliopanwa kwa muda mbele ya tarehe ya sheria hii.

«Wakaaji wa asili hawawezi kuondoshwa kwa nguvu kwenye udongo wanao kaa kabla walipwe malipo ya sawasawa na wapewe udongo mwingine wenye upana na bei yenye kulinganishwa na mahali walipo ondoshwa».

«Kukiwa kunyanganywa, kuwe kwa pori iliopanwa ao ilio panwa kwa muda, kuwe kwa haki yenye wakaaji wa asili wanayo juu ya udongo wakaamo ao wanatumia, peza zote zitatumiwa kwa kuwalipa juu ya kunyanganywa uko, zitalipwa na mfuko wa inchi yenyi kutawaliwa ao ya RWANDA—BURUNDI…».

- Amri ya 5:

«Udongo wote unao patikana ndani ya kata inayo semwa ndani ya amri ya 3 inabaki ya watawaliwa ao ya RWANDA-BURUNDI.»

«Hazi wezi kupanuwa ao kupewa kwa muda; haziwezi kutumiwa umbali mbali na shabaa ya offisi, sawa vile imeoneshwa ndani ya amri ya 2 ya sheria hii».

Kutokea amri mbili hiyo imeonekana kama eneo zinazo wekwa pori za taifa juu ya ufugo ya Virunga, ya Garamba, na ya Upemba zilitoshwa haki zote za watu wengine. Lakini, kwa muundo ya pori za taifa juu ya ufugo ya 1970, ili kuwa ya muhimu kupitia kwa mwenendo unao wekwa na sheria ya 1956 juu ya kunyanganywa kwa sababu ya matumizi ya watu wote.

Kwa yenye kuangalia akiba tatu ya maisha ya ulemwengu, kuona tahere yao ya muundo, kwa kuziacha uhuru na haki zote za watu wengine ilipashwa kufwata mwenendo ya kunyanganywa kwa sababu ya matumizi ya watu wote inayo toka kwa sheria no 77-001 ya 22 Februari 1977.

### *II.4. Misitu Za Kupangwa Zilizo Undwa Na Sheria Ya Waziri, Amri Ya 15 Sheria Ya Msitu*

Amri ya 10 cha sheria ya pori Kinapanga: «Milki ya pori inakuwa: msitu za kukingwa na pori za kutoa mazao daima».

Yenye kuvuta mafunzo hii ni pori za kupangwa. Izi za mwisho zinatiwa kwa yote chini ya sheria yenyi kutia mipaka ya uchungo na naraka ya kupanga. Kwa kweli, mwenendo ya kupangwa kwa pori ina hakikisha mipaka yake na inatia mipango ao kanuni ya ujenzi na ukingo.

Pori za kupangwa zina weza patikana iwe ndani ya eneo ya kukingwa sawa vile akiba maumbile mzima, pori za taifa, akiba za yote ya maisha ulimwenguni, iwe inje za eneo inayo tajwa. Matumizi zao zina heshemu kanuni muhimu za eneo za kukingwa.

Kufwatana na amri ya 7, nucta c, ya sheria tarehe 26 Novemba 1934 inayo angalia kanuni ya ndani ya offisi ya pori za taifa juu ya ufugo, imekatazwa ndani ya akiba maumbile mzima kukata, kuongowa, kuharibu ao kuondoa minea ao miti zinazo pandwa…

Ina somwa ndani ya amri ya 5 cha sheria ya Raisi 69-041 ya 22 Agosti 1969: «Bila kuvunja sheria makamu isipokuwa ya kawaida ao nyaraka inayo unda akiba nzima, ina katazwa ndani ya akiba nzima…3° kukata, kuharibu, kuondoa ao kuondosha minea ao miti yenye hazi kupandwa».

Ndani ya kitabu cha sheria ya pori, amri ya 38 na 39 inapanga ifwatayo:

- «Ndani ya pori za kupangwa, ikitoshwa tu akiba maumbile nzima, pori za taifa juu ya ufugo na bustani za mimea, haki ya kutumia inatumiwa kwa upekee na wakaaji wa kandokando tu na furaha yao inaomba mbele wa heshimu mipangilio ya sheria hii na vipimo vyake vya matumizi», amri ya 38;

- Ndani ya pori za kupangwa, haki za kutumia yana mipaka:

    1. Kwa kuogota kuni na majani;
    2. Kwa kuchuma mbegu, za mimea ao za kutumia kwa chakula ao matunzo;
    3. Kwa mavuno ya matonvu mbalimbali ao asali;
    4. Kwa kuogota vidudu vinavyo tumiwa kwa kula, kola ao vyura;
    5. Kwa kuchaguwa miti inayo saidia kwa majengo za nyumba.

«Juu ya yote mpango wa ujenji wa kila pori inao pangwa inatokana na haki za kutumia inayo ruhusiwa kwa pori za kupangwa», amri ya 39.

Sehemu hii ya mwisho ya amri ya 39 inapashwa matumizi yake ndani ya vipengele vya 6 na 7 ya sheria ya Waziri no 034/CAB/MIN/ECN-T/JEB/08 tarehe 22 Agosti 2008 inayo sema juu ya kanunisho ya mavuno ya mazao moja za pori.

- «Mpango wa ujenzi ya pori zote za kupangwa inaweka namna za mavuno ya mazao za pori yenyi inapashwa fanyika na wakaaji wa jirani wa pori kwa msingi wa haki ya kutumia, sawa vile mavuno, kutajwa na kuhesabiwa pia vile eneo na wakati wa kuondoshwa kwa mazao; mwenye mamlaka ana uwezo wa kuvunja mpango kama inaonekana kuvunjwa ao kuto heshimu moja ya juu, amri ya 6;

- «Imekatazwa kuuza mazao yote ya pori zinazo vunwa ndani ya pori inayo pangwa kwa haki za kutumia», amri ya 7.

Inatoka waziwazi kwa vipengele vyote hivi kama pori zinazo patikana iwe ndani ya akiba maumbile nzima kama vile ndani hifadhi ya taifa, ni kusema ndani za eneo za kukingwa hazipo za kuguswa. Ikiwa sheria inajua haki za kutumia kwa wakaaji wa jirani tu za pori za kupangwa zinazo patikana inje ya eneo za Kukingwa, haki za kutumia hizo zina pashwa kulazimishwa kukanunishwa ndani ya mpango wa ujenzi ya pori ya kupangwa ya yote. Mazao zote za mavuno ndani ya pori ya kupangwa inapashwa kutumiwa na mwenye kuvutwa na jamaa lake, ndio maana imekatazwa kuuza.

Sheria ya Waziri no 08/08 ya 8 Aprili 2008 ina onyesha mwenendo wenye kuwa na shabaa yake, pori za kupangwa. Ndani ya mwenendo huu, ujuvi mbele ya yote wa watu wote na ya muji (kijiji) na wakaaji jirani wa pori kwa upekee ni muhuri kwa jumla kama ilivyo mawazo ya kamati ya ujuvi ya jimbo inayo husika na pori.

Sehemu ya 2 ya amri ya 10 ya sheria ya Waziri kinapanga:

«Kama ujuvi inasema kwa mwisho kama ni ya muhimu wakaaji wa jirani wa pori wa mahali mengine inje ya makao yao wanao zoea, mapatano yanayo onesha kwa sehemu yalio juu :

1. Inaonekana kukubali kwa haraka kwa kiongozi cha nafasi na kwa hao wajumbe wa wakaaji wa nafasi na/ao wakaaji wa asili wanao angaliwa na mpango huu;
2. Inafafanusha mpango wa kustarehe wa mpya kwenyi hawakujitakia, kwa wakaaji wanao elekewa na namna ya kuyafatilia;
3. Inaonyesha sharti zilio za mbele na mwenendo wa kustarehe kwa mpya huku;
4. Kuandika malipo yatakao pewa wakaaji kwa ajili ya kuwapa makao mapya na kuyatumikisha;
5. Kujulisha ginsi wakaaji wanaweza kufanya ombi lao wakati mipango ya kuwapa makao mapya haya heshimiwe yote ao kwa sehemu…».

Kwa yote yanayo angalia malipo na kupewa makao mapya, wakaaji wote wa kandokando ya msitu uliopangwa kwa kuacha huru msitu huu, kufuatana na haki zote za msitu wa mazoezo.

### *II.5. Siasa Ya Mazingira Ya 15/100 Ya Eneo Lote La Udongo Ya Inchi Inayo Semwa Katika Amri Ya 14 Ya Buku La Sheria Ya Msitu Ina Maana Gani?*

Amri ya 14 ya kitabu cha sheria la msitu kinasema: «Msitu uliopangwa unapashwa kukamata ukiwa mdogo eneo la 15/100 ya yote ya udongo wa nchi». Shabaa ya 15/100 yanatoka katika masemi ya Raisi Mobutu ya tarehe 9 Septemba 1075 ya N'sele.

Tukiangalia kwa mara ya pili muhtasari unao elezea unasema: «Katika muda wa miaka kumi, tumeunda hifadhi ya taifa na akiba maumbile kuliko katika miaka

makumi nane ya utawala wao. Na shabaa letu ni kufikia kwa ukingo wa msitu wote ulio katika 15/100 ya eneo la nchi na ni ya mafaa, tukiangalia ukubwa wa Zaïre…».

Ndani ya masemi ya Raisi wa Jamhuri, inasema kwa ajili ya eneo zinazo kingwa kwa tafsiri nzuri, yanaonesha kwamba; msitu uliopangwa unapatikana ndani.

## *II.6. Fasi Ya Shirika La Wakaaji Mahali Katika Buku La Sheria Ya Msitu*

Mwandishi ao mtunga sheria juu ya msitu anasema: «Kikundi cha wakaaji wa nafasi», mara kumi[16]; masemi «Wakaaji wa kandokando», mara tatu[17]; masemi «Wakaaji wa nafasi», mara mbili[18]; na masemi «Kijiji cha kandokando», mara moja[19].

Kwa yale yanayo angalia masemi haya, waandishi V.Vundudia na Massamba na G.Kalambay Lumpungu (2009) katika kitabu cha sheria ya msitu iliyo tafsiriwa na kuwekwa mkazo wanaandika: «Kwa namna moja, masemi kikundi cha wakaaji wa nafasi hawawezi kufanishwa na neno kikundi cha "wakaaji wa miji". Ao tena na neno "wakaaji wa kandokando ya msitu fulani". Mji mumoja na mkusanyiko wa watu wanao makao pamoja na/ao wenye kuchangia kilimo na kwa hiyo inaweza kukaamo watu walio wa vikundi mbalimbali vya wakaaji wa nafasi. Lakini, kikundi cha wakaaji wa nafasi kinaweza kupitia hesabu ao wingi wa wakaaji kuwa na vijiji vingi. Kundi la wakaaji wa nafasi wanaweza kuwa wenyeji pori fulani na kwa hivyo wataitwa wakaaji wa kandokando ya pori hii; lakini, wakaaji wote wa kandokando ya pori fulani hawapo hakika wakaaji wa nafasi kwa sababu; kwa faida fulani za kufaa kwa ushirika na uchimi; watu wanao toka katika vikundi mbalimbali vya wakaaji wanaweza kuishi pamoja ndani ya eneo ilio ya pori»[20].

### II.6.1. Mwanzo wa jina «wakaaji mahali» katika sharia ya wa kongomani

Neno «wakaaji wa nafasi» lilitumiwa kwa mara ya kwanza katika sheria inayo angalia pori katika amri ya 387 na 388 bila kutafsiriwa. Giza hiyo ilitoshwa kwa sehemu na mtunga sheria ya pori kwa amri ya 1, sehemu ya 17 kwa maneno haya:

[16] Amri ya 1, 17, 22, 78, 79, 80, 89, 106, 111, 112, 113.
[17] Amri ya 15, 38, 44.
[18] Amri ya 62, 102.
[19] Amri ya 63.
[20] Vundu dia Massamba et G. Kambay Lumpungu, buku la sheria ya pori inayo tafsiriwa na kutiwa mkozo, ukurasa 8.

«Kundi la wakaaji wa nafasi: ni wakaaji wa nafasi, ni wakaaji ambao wapo chini ya uongozi wa mazoezo na wanao ungwa kwa masikilizano ya vikoo ao ya vizazi ambavyo vinatia nguvu, umoja wao wa ndani. Wanajulikana tena kupitia udongo ambamo wanakaa.»

Kundi la wakaaji wa nafasi linaangaliliwa pia na namna wanavyo ishi na kuongozwa. Ona namna gani sheria ya ndani no 08-016 ya tehere 7 Octoba 2008 inayo angalia, muundo, matengenezo na namna ya matumikio vya sehemu zinazo achana uongozi na mapatano yao na serikali na jimbo ndio inaleta tofauti kati ya secteur na chefferie.

- «Ufalme wa secteur ni mkusanyo wa vikundi vya wakaaji wa asili mbalimbali na waliohuru, waliochini ya uongozi wa mazoezo waki ongozwa na sultani aliye chaguliwa na kupewa mamlaka na serikali.»

«Imeongozwa kufwatana na mipango ya sheria hii. Kwa yote, vikundi vya ufalme wa vizazi vya asili vilivyo ndani yake, wanabaki kila kikundi na maongozi yao ya mazoezo, waki heshimu mipaka na kanuni zilizo ndani ya sheria hii na ya sheria inayo angalia usultani wa asili», amri 66[21].

- «Chefferie ni mchango wa vikundi vya wakaaji wa asili moja, wanao ongozwa kufwatana na mazoezo na vilivyo chini ya utalawa wa kiongozi anaye chaguliwa na asili.»

[21] Kufafanisha:
- Sheria no 95-005 ya tahere 20 Decemba 1995 juu ya mgao wa utawala wa serikali, amri ya 107.

«Collectivite secteur ni sehemu ya uhakimu ndogo inayo chunga vikundi vidogo vidogo vya asili mbalimbali na vilivyo huru, vinavyo ongozwa kufwatana na mazoezo, vinavyo wakaaji wadogo kwa ajili ya maendeleo yao na wanao sultani anayejulikana na kupewa mamlaka na serikali».
«Collectivite secteur ina uhakimu kufwatana na mipango ya sheria hii kwa yote, vikundi vya ufalme wa vizazi vya mazoezo vilivyo ndani yake, wanachunga asili yao kufwatana na mipaka na kanuni zilizo ndani ya sheria hii».
- Sheria makamu 081 ya tahere 2 Julai 1998 inayo angalia mpango wa udongo na uhakimu, amri ya 140.

«Secteur ni jumla ya vikundi vidogo vidogo vya wakaaji mbalimbali wa asili zilizo huru, inayoongozwa chini ya mazoezo, lakini ambavyo vina wakaaji wadogo kwa ajili ya maendeleo yao mazuri na iliyo chini ya uongozi wa sultani anaye julikana na kupewa mamlaka na serikali: Imeongozwa kufwatana na mipango ya sheria makamu hii. Kwa yote, vikundi vya falme za vizazi na mazoezo vinavyo patikana ndani yake, vinachunga kila moja namna yao ya maongozi, vikiheshimu mipaka na kanuni zilizo katika sheria hii».

«Imeongozwa na uhakimu kufwatana na mpango ya sheria hii na yamazoezo, ikiwa mazoezo hii hayako tofauti na sheria, na yote yalio andikwa; pia na amani na tabia nzuri», amri ya 67[22].

Kupitia matafsirio mawili, imeonekana kwamba kikundi cha wakaaji wa nafasi kina fananishwa na vikundi vya wakaaji wa asili walio chini ya uongozi wa sultani fulani. Kwa hayo, sheria ya ndani ya tahere 7 Octoba 2008 inasema kwa amri ya 85 kwamba, sultani wa secteur ni kiongozi cha secteur, na kwa iyo, yeye ni mjumbe wa secteur mbele ya vyumba vya haki ya watu wengine. Kwa yenye kwangalia kiongozi cha chefferie, amri ya 86 ya sheria hii moja inasema kwamba: «sultani wa chefferie ni kiongozi cha chefferie, yeye ni mjumbe wa chefferie mbele ya chumba cha haki na mbele ya watu wengine».

Kwa mambo yanayo angalia sultani wa asili, kipengele cha 207 sehemu ya 1 na ya 2 ya katiba inasema: «Kiongozi wa asili anajulikana. Umeongozwa kufuatana na mazoezo ya nafasi, ikiwa hayabishane na katiba, sheria, amani na tabia nzuri…».

Kufuatana na kweli ya maisha, vikundi vya wakaaji wa asili wanaonyesha uhai wao kupitia miji na vijiji kwa hiyo, amri ya 142 cha sheria ya tarehe 20 Desemba 1995 na amri ya 161 ya katiba cha tarehe 2 Julai 1998 vinasema: «inaitwa mji, kikundi chote cha wakaaji wa asili wanao ongozwa na mazoezo ao na asili ya nafasi na ambayo umoja na mapatano ya kati imejengwa kufuatana na msingi ya undugu wa vikoo na vizazi».

---

[22] Fafanusha:

- Sheria no 95-005 ya tahere 20 Decemba 1995 inayo angalia mgao wa inchi kwa uongozi, amri ya 106.

«Chefferie ni sehemu ya uhakimu unao heshimu mgao wa inchi kwa uongozi, inayo kuwa jumla vikundi vya wakaaji wa asili zinazofanana ao moja, inayo ongozwa na mazoezo na iliyo chini ya uongozi wa sultani wa asili anaye chaguliwa kwa mazoezo, anajulikana na kupewa mamlaka na serikali».

«Imeongozwa na uhakimu kufwatana na mazoezo, bila kwa inje ya mipango ya sheria hii na pia mazoezo hii, isiwe umbalimbali na mipango za sheria ya watu wote, amani na tabia nzuri».

- Sheria makamu 081 ya tahere 2 Julai 1998 inayo angalia maongozi ya inchi na uhakimu, amri ya 141.

«Cheferie ni jumla ya vikundi vya wakaaji wa asili zinazo fanana ao moja, wanao ongonzwa kufwatana na mazoezo na ilio chini ya uongozi wa sultani anayewekwa na asili, anaye julikana na kupewa mamlaka na serikali».

«Imeongozwa na uhakimu, kufwatana na mazoezo, bila kwenda umbalimbali na mipango ya sheria makamu hii, na pia mazoezo hii, yasiwe umbalimbali na mipango ya sheria, na amani na tabia nzuri».

Kikundi chote cha wakaaji wa nafasi ao kikundi cha wakaaji wa asile ni wenyeji wa sehemu fulani ya msitu, sehemu hii iliyo mali ya watu wote ina angalia udongo na yote yapatikanamo kama ville maumbile, na msitu. Kikundi na wana memba wake wana uwezo unaohesabika juu ya sehemu hii ya udongo, kama vile haki pori maumbile na ya vipimo mbalimbali. Wana memba wa kikundi hiki cha wakaaji wana wote kwa ujumla haki moja ya kutumikisha. Haki hizi ni ya upekee, ni kusema mtu wote anae makao katika sehemu hii ya udongo ya kikundi cha wakaaji; akiwa yeye mwenyewe, ana haki ya kuondoa ao kutumikisha faida yote ambayo sehemu hii ya udongo inaweza kumtolea kama vile kuwinda, uvuvi, mavuno ya manufaa, maumbile na kadhalika…Ni lazima kujulisha kwamba uhuru na matumikisho yote ya haki ya upekee aliyo nayo juu ya sehemu hii, inaonesha kwanza kwamba mtu huu ni moja wa kundi la wakaaji walio wenyeji wa sehemu hii ya msitu.

Kwa yenye kuangalia sehemu ya msitu ya wakaaji fulani wa nafasi ao wa asili wanaweza kuishi ndani yake, si wana memba tu wa kikundi cha wakaaji hawa, lakini pia watu wanao ungana na kikundi hiki cha wakaaji kwa njia ya unyumba, kuingizwa katika jamaa kwa ulezi ao kwa mbinu zote za mazoezo, pia tena wageni. Katika matumikisho ya haki za kufurai kwa watu wote, hakuna tafauti kati ya wana memba wa kikundi cha wakaaji, mwana memba aliye ingizwa na mgeni; lakini tofauti inakuwa kubwa katika umbo la sheria la kuondoshwa haki. Kwa hiyo ikiwa wote wana ruhusa ya kutumika katika udongo, ukingo na ustawisho wa matumizi ambayo vikundi mbalimbali ivi vinatoa, yaenda kutoka ukingo mkubwa hata kukosewa ikiweza kukubaliwa.

Amri mbili vya kitabu cha sheria ya msitu inatafsiri yote ambayo yanatoka kusemwa:

- «Miti zilizo ndani ya miji ao mazingira yake inayo fuata ao ndani ya shamba ya watu wote ao ya upekee ni ya watu wote wa miji ao ya mwenyeji shamba», amri ya 9, sehemu ya 1.

- «Kundi fulani ya wakaaji wa nafasi kupitia ombi lao, wanapewa ruhusa ya kutumikisha eneo fulani kwa sehemu ao lote la msitu ulio kingwa kati ya msitu wanazo zitumikisha kufuatana na mazoezo», amri ya 22, kipengele cha 1.

Amri ya 111 mpaka 113 vinasemea namna ya kutumikisha misitu zilizo pewa kwa vikundi vya wakaaji wa nafasi.

### II.6.2. Haki za matumizi ndani ya misitu zenye kupangwa

Amri ya pili imetafsiri haki ya matumizi ndani ya misitu zilizo pangwa.

- Amri ya 38:

«Ndani ya misitu zilizo pangwa, kutosha akiba ya maumbile yote, hifadhi ya taifa na shamba ya miti ya ufugo, haki za matumizi zina pewa tu kwa wakaaji wa kandokando na uhuru wao wakitumikisha ku fuatana na heshima ya mipango ya shria hii na ya namna yake ya matumizi».

- Amri ya 39:
  «Ndani ya msitu uliopangwa, haki ya matumizi ina mipaka ifuatayo»:
  a. Kwa kuogota kuni na magungu;
  b. Kwa kuchuma mbegu, mimea ya malisho ao miti ya dawa ;
  c. Kwa mavuno ya bulimbu, mbegu ya resin ao asali;
  d. Kwa kuogota vidudu vya malisho, kola ao vyura;
  e. Kwa kuchagua miti ya majengo ya makao na ya matumizi ya asili.»

«Pia, mpango wa matengenezo ya kila msitu ulio pangwa, unajulisha haki za matumizi inayo ruhusiwa kwa msitu wa kupangwa».

Haki ya matumizi ndani ya msitu uliopangwa inajulishwa kufuatana na hali ya sasa ya uchumi, asili na maendeleo ya nafasi pia kuondoshwa kwa haki haya yote inaweza kutofanyika ao kuwa ngumu kutumiwa. Kwa sababu wakaaji wa kandokando wanafaida katika matumizi ya manufaa ya lazima kwa kusaidia faida ya maisha yao.

Sehemu ya kwanza ya amri ya 39, inafanana katika matungo yake, inayo onesha kwamba, namna ya yote inayo tajiwa ndani yake ina mipaka. Lakini sehemu ya pili inaeleza mamoja na sehemu ya kwanza. Kwa hiyo, mpango wa matengenezo unaweza kupanusha haki zake kufuatana na uwezo wa msitu huu ulio pangwa.

## *II.7. Muhimu Wa Sheria Na Wa Vyumba Vya Mamlaka*

Katika kipindi hiki, tutaonyesha naraka ya sheria na ya vyumba vya mamlaka inayotajwa katika mafunzo haya.

### II.7.1. Chumba cha sheria

Amri ya 9 ya katiba ya tarehe 18 Februari 2006 na ya sheria zote zilizo kamatwa.

Kwa hiyo, kwa kufikia shabaa zinazo kusudiwa kwa yote yanayo angalia ukingo wa mazingira yafaa kutia kanuni zinazo julikana kwa matumikisho ya kazi zinazo pashwa kuanzishwa.

#### *II.7.1.1. Matokeo ya amri ya 9 ya katiba ya tarehe 18 Februari 2006*

Amri ya 9 ya katiba ya tarehe 18 Februari 2006 kinasema:

«Serikali ina mamlaka kwa wakati wote juu ya udongo, yote yalio chini ya udongo, maji na msitu, juu ya anga, mito mikuu, boma na bahari ya Kongo pia na vilima vyote vya bara».

«Namna ya matumikisho na ya kupanwa kwa yote ya serikali kama inavyo onyeshwa katika sehemu iliyo tangulia ya amri hii, imepangwa na sheria».

Sehemu ya kwanza ya kipengele hiki inasema kwa jumla matumikisho kwa namna sheria za inchi zote zinasema: uhuru wa taifa ao inchi moja moja juu ya msitu ao udongo wake. Ona yanayosemwa na Nicolas De Sedeleer katika «Vade-Mecum yake juu ya sheria inayo angalia inchi zote kwa yote yanayo leta maisha mbalimbali-Wilaya-Africa» : «Kwa ajili ya upingaji uliodumu kati za inchi ya kaskazini na ya kusini kwa yale yanayo angalia kuzipa mambo moja moja ya yote yanayo angalia mafunzo mbali mbali ya yote yanayo angalia maisha kwa upekee (genes), mafunzo juu ya mali ya kuchangia ya ulimwengu mzima ilionekana kuwa msingi wa mabishano ao wa kurudilia wakati wa mkutano wa Rio. Pia ya kuachwa na wandishi wa kitabu la masikilizano juu ya umbali mbali wa mafunzo ya yote yanayo leta maisha kwa faida ya neno "yanayo husika na watu wote". Kwa faida hili moja, neno uhuru unaodumu na ulio wa jumla wa kila inchi juu ya manufaa maumbile yake[23] ilijihakikisha wakati wa mkutano wa Rio. Katika maongezi ya sehemu ya pili ya mpango huu unao tangaza kwamba "inchi zina haki ilio huru ya kutumikisha manufaa yao kufuatana na siasa ya mazingira na maendeleo"»[24].

[23] Ni sisi tunatia mihstari.
[24] Nicolas de Sadeleer, Vade Mecum juu ya sheria ya inchi zote inayo angalia yote yanayo maisha ukurasa wa 19.

Kufuatana na uhuru wake unaodumu na ulio wote tangu tarehe 30 Juni 1960, serikali ilikamata sheria hizi:

- **Udongo:**

  - Sheria n° 73-021 ya tarehe 20 Julai 1973 inayo angalia namna ya matumikisho mpango kwa jumla ya vitu, mpango wa msitu na wa yote yanayo dumu na mpango wa ukingo.

    - «Eneo lote la kitanda cha mito mikuu na vya lindi zote zinazo weza kutembelewa na mashua inayo tembea ao hapana ni ya serikali», amri ya 16;
    - «Maji ya mito na ya vilindi na maji ya chini ya udongo ni ya serikali», amri ya 18;
    - «Udongo ni wa serikali tu, hauwezi kugawa wala kuondoshwa», amri ya 53.

  - Sheria makamu n° 69-041 ya tarehe 22 Agosti 1969 juu ya umbo:
    - «Sehemu zote za udongo wa inchi wa jamhuri unaweza kuwekwa na sheria kuwa "Akiba maumbile nzima".Wakati akiba ya wanyama ya msitu, ya udongo, ya maji na kwa jumla ya nafasi maumbile fulani inalazimisha faida ya lazima na ikiwa inaomba kuondoa nafasi hii kwa matumizi yote inayoweza kuyaregeza ao kubadili hali, mchango ao namna na maendeleo», amri ya 1.

  - Sheria n° 75-024 ya tarehe 22 julai 1975 inayosema juu ya sehemu zilizo chungwa:
    - «Sehemu zote za pori ya inchi isiyo funikwa na mpango wa kujenga miji mikubwa inaweza kusimamishwa, na sheria ya raisi wa Jamhuri kuwa "sehemu ya kuchunga", wakati yanatoa faida inayo onesha ulazima wa kuweka akiba, kutengenezwa ao kuyatumikisha», amri ya 1.

- **Yaliyo chini ya udongo:**

  - Sheria makamu n° 81-013 ya tarehe 2 Aprili 1981 inayo angalia mipangilio kwa jumla ya sheria juu ya madini na mafuta yote:

    - «Kufuatana na mipango ya katiba, yote yalio chini ya udongo wa Zaïre na inaendelea kuwa ya taifa. Na inakuwa na: madini, eneo zinazo mali

ya chini ya udongo, visima vya maji ya kunywa na mafuta…», amri ya 1, sehemu ya 1.

- Sheria n° 007-2002 ya tarehe 11 Julai 2002 inayosema juu ya kitabu cha sheria ya madini:

➢ «Mahali panapo patikana madini, na pia mahali panapo lindwa madini, maji ya chini ya udongo na makao madini yapatikanayo mengi inayo patikana juu ya eneo ya udongo ao chini ya udongo ao katika mito ya udongo ya inchi ni ya serikali tu, isiyoweza kupanwa wala kuondoshwa», amri ya 3 sehemu ya 1.

- **Mazao maumbile:**

- Sheria n° 82-002 ya tarehe 28 Mei 1982 inatia mpango juu ya mawindo:

➢ «Akiba ya wanyama ni mchango wa wanyama wote wa msitu wa namna mbalimbali na aina zote zilizo na mifupa na zisizo na mifupa yanayoweza kunyonyesha, ndege inayo tembea ndani ya ganda mijusi na aina zote za wanyama wa msitu. Umoja wa wanyama wa Zaire ni ya serikali. Ni mali ya taifa na yana pashwa kutumikishwa ao kutumiwa kwa faida ya taifa», amri ya 2.

- **Mito ya inchi ya Kongo:**

- Mipaka ya eneo la mito ya Jamhuri ya Kidemokratia ya Kongo iliunda sheria n° 09/002 ya tarehe 07 Mei 2009 inayo angalia mipaka ya eneo la maji ya Jamhuri ya Kidemokratia ya Kongo. Amri ya 8 sheria hii kinasema:

➢ «Vilindi vya bara vinakamata eneo mpaka elfu 350 ya urefu wa eneo la maji tangu mustari wa maanjilio mpaka elfu 100 ya upana wa eneo la maji wa meta 2.500.»

### *II.7.1.2. Uwezo wa kurudilia mipango ya kale ndani ya sheria ya misitu*

Imejulikana kwa jumla kwamba katika haki, sheria inauwezo juu ya mambo yatakayo kuja, walasi juu ya mambo yaliyo pita mbele ya kukamatwa kwa sheria.

Sheria n° 73-021 ya tarehe 20 Julai 1973 inayo angalia matumizi kwa jumla ya vitu, matumizi ya pori na vyote visivyo tembea na matumizi ya ukingo inakuwa na sheria lake katika amri ya 14 bis ya sheria no 71-008 ya tarehe 31 Dicemba 1971 inayoangalia mkaguo wa katiba ya 1967, sheria inayosema katika amri ya yake ya

kwanza: «imeongozwa katika ya amri ya 14 bis kinachosema hivi: “udongo na yote yapatikanayo chini ya udongo wa Zaïre pia na mazao maumbile yote yapatikanamo ni ya serikali.”»

Kufuatana na amri ya 53 ya sheria juu ya pori kinacho hakikisha uwenyeji wa pori kwa serikali tu, iliomba kwa wa Kongomani, wageni na kwa viwanda vyote vya serikali ao vya upekee vilivyo kuwa na haki ya uwenyeji wa pori waliopewa kwa kawaida mbele ya kutumikishwa kwa sheria juu ya pori, kuyabadilisha kwa haki ya ruhusa ya kutumikisha kunako endelea ikiwa ni mkongomani, na kwa ruhusa ya kupewa kwa kutumikishwa ya kawaida, ikiwa ni mgeni ao kiwanda cha serikali ao cha upekee.

Kufuatana na mamlaka ya amri hii moja ya 53, udongo ulio wa vikundi vya wakaaji wa nafasi, ulikubaliwa kuwa sehemu zilizo na wenyeji amri ya 387 na ahadi ya kutengeneza haki ya matumikisho iliyo pewa kwa usawa kwa vikundi vya wakaaji hawa juu ya udongo wanayo yatumikia na mahali walio jengwa kufatana na amri ya 388.

Kwa mwisho serikali peke yake tu, katika Jamhuri ya Kongo ndiye mwenye pori.

#### *1.7.1.3. Naraka mbili*

Kufuatana na haki juu ya mazingira imepelekua katika chumba cha wabunge. Wakati yatakubaliwa, itakuwa lazima na mamlaka juu ya sheria inayoangalia mazingira. Inakuwa sheria ya ndani juu ya mazingira na sheria mpya juu ya akiba ya umbo. Matumikisho ya sheria inapaganishwa juu ya naraka nyipya, tukiangalia hali ya mwanzo na ilio na matatizo mengi ya matumikisho ya sheria.

Kutela kwa Jamhuri ya Kongo sheria ya ndani, ambayo inahesabu kanuni kwa jumla za sheria kwa yote inayoangalia maziringira, bila kwenda inje na faida za sasa za utaalamu na ya mapatano ya inchi zote zilizo tiwa saini na Kongo, kwa kuwa ni ya lazima.

Kwa ajili ya kanuni ya ma ambatano ya namna, ni lazima chumba cha bunge kivunje sheria – makamu n° 69-041 ya tarehe 22 Agosti 1969 inayo angalia akiba ya umbo. Kwa hayo, tunasoma katika katiba, «Bila kuharibu mipango mingine ya katiba hii, sheria ana hakikisha kanuni kuu zinazo angalia…ukingo wa mazingira na wa kutembea...», amri ya 123, nukta ya 15.

Mbele ya kuacha mezani pa chumba ya ubnge mafikiri ya sheria, chumba cha wa kongomani kinacho husika na akiba ya umbo kilitengeneza vikao tano vya

kufikiria vinavyo badili majimbo yote pa Mwanda, Lubumbashi, Goma, Kisangani na Mbandaka.

Mafunzo ya ndani ya mpango ya sheria makamu hii inafumia kwamba mipango hizi zi nasema kwa sehemu na zinatumiwa tu kwa ajili ya akiba zote na hapana kwa eneo zinazo kingwa. Haya kubaliane hata na mkataba wa mapatano za inchi zote yanayo angalia utofauti wa masomo ya yote yanayo maisha na kwa kanuni na sheria nyipya ya matumikisho ya mafunzo mbalimbali ya yote yanayo maisha,ya eneo zilizo kingwa za eneo ya kutoa maji. Hivyo, ni lazima sana na mambo mengi yanalazimisha mabadirisho haya ya sheria.

Mradi ya sheria ungetaka:

1. Kutoa hali ya jumla na ya mchango, kusudi yote yanayo angalia akiba ya yote yanayo maisha mbalimbali na pia katika sehemu zinazo onekana bila faida;
2. Kujulisha kwa wazi sehemu za mamlaka ya kila moja kati ya wale wanao uwezo leo na kesho katika akiba ya umbo;
3. Kuingiza katika kanuni na mipango yanayo sema juu ya maneno haya, inayo andikwa katika buku ya masikilizano ya mataifa yote ambayo inchi zote zilikubaliana;
4. Kujibu kwa ombi za maendeleo daima kwa faida ya vikundi vya wakaaji wa nafasi na ya wakaaji wa asili;
5. Kuingiza wote walio katika makubaliano haya, na kuheshimu maneno yote mapya yanayo toka katika masikilizano mapya juu ya akiba yanayo dumu.

### II.7.2. Msingi unao husu vyumba vya madaraka

Haiombi tu mafasirio ya haki ya uwezo wa watu wote kwa kutumikisha kazi zilizo zake. Inafaa pia matumikisho ya watu wote ipangwe mipango za sheria ao zakuongoza inayo hali ya vyumba vya mamlaka tangu sasa zinapashwa kuwa:

1. Kugawanya mamlaka kwa viongozi mbalimbali wa inchi;
2. Kuunda kazi za uhakimu, kusimamisha vyumba vya kazi vya watu wote na kugawa kazi zao;
3. Kupanga namna mbalimbali zitakazo simamia ao kutumikishwa kwa kazi hizi na vyumba hivi, kuongoza matumikisho ya mamlaka yao na inayo akikisha kuchungwa kwa haki ya wanao ongozwa;
4. Kutoa mali za lazima kwa maendeleo ya kazi yao.

Kwa jinsi shabaa kubwa ya majifunzo haya ni kwa ajili ya pori zilizo pangwa, akiba zote na akiba ya wanyama ni lazima katika nukta hii kuonyeshe aliye na uwezo juu ya hayo.

### *II.7.2.1. Chumba cha waziri kinacho husika na mazingira, akiba ya umbo na matembezi*

Sheria 75-231 ya tarehe 22 Julai 1975 inajulisha kazi ya chumba cha Waziri kinacho husika na mazingira, akiba ya umbo na matembezi katika maneno haya:

- «Chumba hiki kina uwezo wa kuendelesha na kutumikisha kazi zote zinazo angalia mazingira, akiba ya umbo, kutembea, na nyumba vya kupangisha watu na kukamata mipango zote na sheria zinazo ruhusu kutimiza kazi hii yote, kufuatana na maendeleo ya sasa ya utaalamu. Chumba hiki, kimipewa uwezo wa:

**1.** Katika miji mikubwa:
- Usafi wa makao ya watu kwa njia ya kupiganisha yote yanayo kuwa hatari inayotoka kwa uharibifu wa maji, wa udongo na wa hewa;
- Kuunda vyumba vya kazi vya watu kwa njia ya kutengeneza msitu ao kukinga hifadhi ya taifa, wakitumikisha siasa ya kupanda miti na ya kupiganisha maporomoko ya udongo;
- Kuleta mawazo juu ya mambo yanayo angalia kuundwa kwa miji mikuu na ya yote yanayo angalia makao;
- Kutoa mawazo yanayo ombwa juu ya mpango wowote wa kutia viwanda via kazi na wa matengenezo yanayo weza kutengeneza ao uharibifu wa maisha.

**2.** Katika miji na vijiji:
- Kuunda na kutumikisha akiba maumbile, ya yote na yalio karibu na ya hifadhi ya taifa, akiba ya mawindo, ya uvuvi na ya manufaa yanayo toka katika maji;
- Kuhakikisha ukingo na hifadhi ya wanyama na ya msitu katika akiba hizi;
- Kuunda na kutumikisha viwanda vilivyo kwa ajili ya «kubamba, kukamata» vinavyo jengwa ndani ao nje ya akiba;
- Kuunda na kutumikisha yote yanayo angalia maisha katika maji na katika msitu.

**3.** Kwa yote yanayo angalia matembezi na nyumba ya kupangisha watu:

- ➢ Kuendeleza yote yanayo angalia matembezi katika inchi ya Zaïre kwa njia zote zinazo faa kama vile: kuyaelezea watu wote, kuunda offisi ya majuvio juu ya matembezi na kutengeneza nafasi ya kupokea watembeaji;
- ➢ Kuendeleza na kupanga kiwanda kinacho angalia kazi ya kupangisha kuunda na kutumisha akiba ao mali yanayo angalia kupangisha wageni ao yanao angalia nyumba ya serikali ya kupangisha watu», amri ya 1.

- «Kazi na vipaji vya zamani vilivyo kuwa via offisi ya Zaïre ya matembezi "O.Z.T." pia iliokuwa ya chumba cha taifa juu ya akiba ya umbo "I.N.C.N" imekuwa kwa haki ya chumba cha Waziri kinacho husika na mazingira, kuchunga akiba ya umbo na matembezi.»

Ndani ya sehria mbalimbali ya Raisi na mipango ya Waziri zinazo weka vipaji vya mawaziri kuwa inayo angalia chumba cha Waziri anaye husika na mazingira inafaa kuongeza:

- Matumikishi ya msitu, ya bustani ya wanyama na mimea, matumikisho ya utaalamu unao kuwa kinyume ndani ya mazingira na shirika na matengenezo ya mahali;
- Kukanunisha mawindo na ya uvuvi, kuchungwa kwa nyama na ya majani na miti;
- Utungo wa mipango zinazo angalia usafi wa mahali panapo ishi watu wakitumika pamoja na chumba cha Waziri kinacho husika na afya muhuri;
- Kufatilia na uhakiki mbinu ya ma ofisi ya muhuri na ya upekee inayo tumika juu mambo inayo angalia mazingira na ya kuchunga akiba ya umbo;
- Matumikishi na kugeuza uchafu kwa kuyatumia kwa kazi zingine;
- Utungo wa mipango inayo angalia usafi wa mahali ya maisha ya watu na heshima ya mazingira ndani ya viwanda vya madini, wakitumika pamoja na chumba cha Waziri anaye husika na madini.

### *II.7.2.2. Chumba cha Kongo kinacho husika na kuchunga akiba ya umbo*

Chumba cha Kongo kinacho husika na kuchunga akiba ya umbo kina ukoo unao toka mbali. Kwa kweli, kwa sheria ya Julai 9 1929 iliundwa offisi inayo itwa hifadhi ya taifa Albert. Kufuatana na jina hili, inasemwa ndani ya ripoti ya kuchambua ya mikutano ya kamati utawala ifwatayo: «Amri ya kwanza jina, hifadhi ya taifa Albert inaitwa kwa mara moja chumba kinacho barua ya kukubaliwa na serikali kwa raiya na mitaa inayo wekwa kuwa akiba maumbile inayo kuwa chini ya

kawaida ya upekee». Jina hili lilibadili kwa mwaka 1934, kwa kweli, amri ya 1 cha sheria ya Novemba 26 1934 inapanga:

«Kunaundwa chumba kinatcho itwa: chumba cha hifadhi ya taifa wa Kongo Ubeliji.»

«Chumba hiki kitafaidika na barua ya kukubaliwa na serikali.»

«Makao yake ina wekwa pa brussels.»

«Chumba hiki kinatwaa nafasi ile ilio itwa hifadhi ya taifa Albert na ina chukua haki na sharti zake zote.»

Kufuatana na amri ya 2 cha sheria ya Waziri, chumba kina shabaa ya kuhakikisha ndani ya mitaa zilizo na akiba zake, ukingo wa nyama na wa majani na miti kusaidia mafunzo ya utaalamu pia kuwapa watembezi moyo haya yana patikana na ukingo wa umbo.

Kufuatana na sheria ya Raisi n° 67-514 ya Decemba 1 1967, jina la chumba cha 1934 ilitoshwa kipande chake «Ubeleji» kwa kuitwa «chumba hifadhi ya taifa ya Kongo». Na ili batizwa tena ndani ya sheria ya Raisi n° 69-041 tarehe ya 22 Agosti 1969 kwa kuwa «chumba cha kutunga akiba ya umbo ya Kongo» na ikabaki na shabaa lake, na ikawekwa chini ya ulinzi wa Raisi wa Jamhuri kwa njia ya sheria yake no 69-062 tarehe ya 5 Decemba 1969 (amri ya 4). Ilibeba jina la chumba cha taifa juu ya kuchunga akiba ya umbo. Kufuatana na sheria 75-023 tarehe ya 22 Julai 1975. Ndani ya sheria ya Raisi 78-190 tarehe ya 5 Mei 1978 inayo angalia kanuni, chumba kina shabaa:

«1. Kuhakikisha ukingo wa nyama, majani na miti ndani ya akiba maumbile nzima ao nzima kwa upande.

2. Kusaidia ndani ya mahali hiyo kufanyike mafunzo ya utaalam na matembezi ndani ya heshima ya kanuni inayo unda ukingo wa akiba ya umbo.

3. Kuongoza vipande kanuni zinazo semwa ″Vya kunasa″ vinavyo wekwa ndani ao nje ya akiba», amri ya 3.

Kufuatana na hii sheria ya Raisi, chumba kina wekwa chini ya ulinzi wa offisi ya mazingira, ukingo wa akiba ya umbo na matembezi na ya offisi inayo husika na viwanda vya serikali, kila mmoja akitimiza vitendo vyake ndani ya kipimo cha mapashwa yake ya upekee, amri ya 21, sehemu ya 1.

Kama inaweza onekana, sheria ya Raisi inayo pana matumikishi hifadhi ya taifa kwa chumba haitumie msemwa msitu wa taifa juu ya ufugo, lakini inapana kwa chumba kazi ya kukinga nyama, majani na miti ndani ya akiba maumbile nzima ao nzima kwa kipande.

Kufuatana na mabadiliko ya namna ya kutumikishwa kwa ma offisi ya mihuri, ina somekana kwa amri ya 4 ya sheria ya Waziri no 10-15 tarehe ya 10 Aprili 2010 inayo wekwa kanuni ya offisi muhuri inayo itwa «Chumba cha Kongo juu ya uchungo wa akiba ya umbo», kwa kifupi «I.C.C.N.»:

«Chumba kina shabaa ya kuchunga akiba ya umbo ya eneo la kukingwa ndani na inje».

«Kwa hiyo anapashwa, ikitajwa:

- Yakuhakikisha ukingo wa nyama, wa majani na miti;
- Kupana yote yanayo maisha mbalimbali, akisaidia mafunzo ya utaalamu na kusaidia kazi za matembezi ndani ya yote inayo maisha kufuatana na sheria ya sasa na ndani ya heshima ya kanuni ya muundo wa ukingo wa akiba;
- Kutimiza ao kukamilisha mafunzo, na kuyahakikisha upelelezi kwa shabaa ya utaalamu na vyombo vya kusaidia kwa mafunzo ndani ya yote iliyo kuwa akiba.

Chumba kina wekwa chini ya ulinzi wa offisi inayo husika na kuchunga akiba ya umbo ndani ya mapashwa zake, amri ya 23; na Waziri anatumia madaraka yake ya ulinzi kwa njia ya kuruhusu mbele ya yote, ya kuitika ao kwa njia ya kukataa, amri ya 24.

Kwa hali ya sasa ya nyaraka na usomi wao, chumba cha Kongo kinacho husika na kuchunga akiba ya umbo kina, fuatana na hali yake ya offisi muhuri unao julikana kuwa ya utaalamu na mbinu matumizi ya msitu (misitu ya taifa, ufugo, ya bustani ya wanyama na ya bustani ya mimea, amri ya 5. Na kwa njia ya sheria no 002-DECNT/CCE. 82 tarehe ya 3 Februari 1982, daraka yake iliongezwa akipewa akiba ya nyama na yote inayo angalia mawindo. Kwa kinyume, eneo zingine za kukingwa zina tumukishwa na wanao pewa madaraka walio tajwa na nyaraka zilizo yaunda: vipande vinavyo lindwa, akiba ya yote inayo maisha ndani ya eneo, akiba ya msitu (misitu).

Offisi inayo husika na mazingira, kuchunga akiba ya umbo na matembezi ina uwezo wa kuunda akiba maumbile nzima na kwa kipande chenye matumizi yao inapewa kwa chumba cha Kongo juu ya kuchunga akiba ya umbo.

Kwa ripoti kati ya offisi na chumba, inaandaliwa na amri ya 23 na 24 ya sheria ya Waziri tarehe ya 20 Aprili 2010.

II.7.2.2.1. Sheria kiongozi ya kodi na malipo mbalimbali

Amri ya 41 sheria tarehe ya 10 Aprili 2010 inapanga «bila kuvunja mipangilio ya umbali mbali, chumba kina faidika kikitendewa namna moja na serikali kwa matumizi yake yote, kuwa inayo angalia kodi, haki na malipo zingine mbalimbali yenye kulipishwa, kulipa na kuya leta kwa mfuko muhuri ao kwa mwenyi madaraka.

II.7.2.2.2. Daraka ya chumba

Chumba kinapewa barua ya kuruhusiwa na serikali na kinapaswa kujibu kwa vitendo vyake vyote vinavyo vunja haki ya watu wengine na ni haki yake kupeleka mbele ya vyumba vya waamzi mtu yeyote anaye vunja haki yake. Ndio maana amri ya 17 kinapanga: «vkipengele vya kuomba ao kujikinga mbele ya vyumba vya waamzi vina ingizwa na/ao kuhakikishwa kwa jina la chumba na kiongozi mkuu ao, isipo kuwa hivyo na mkombozi wake ao na mtu yeyote mwingine anaye pewa mamlaka na kiongozi juu ya jambo hilo».

## III. KIFUPI CHA HAKI NA SHARTI YA SHIRIKA ZINAZO ELEKEA: SERIKALI, CHUMBA CHA KONGO KINACHO HUSIKA NA KUCHUNGA AKIBA LA UMBO AO WATUMISHI WENGINE, WAKAAJI NA SHIRIKA MAHALI

### *III.1. Kibao 1 Akiba Maumbile Nzima: Sheria Ya Raisi 69-041 Ya Agosti 22 1969*

| KAZI ZILIZO KATAZWA | RUHUSA KWA YALIYO KATAZWA |
|---|---|
| - Kuingia, kutembea, kupanga, kulala ndani ya akiba nzima, kuingizamo mbwa, mitego, kuwa silaha ya pori umo, kubeba ao kutumikisha humo nyama za mwitu zinazo maisha, ngozi ao vitumba ao mazao ya majani (mimea) isiyo pandwa, amri ya 4;<br>- Kufuata, kuwinda, kuharibu, kuogopesha ao kuleta mchafuko kwa aina yote ya nyama wa mwitu, hata nyama wa hatari, amri ya 5, 1°;<br>- Kukata, kuharibu mayayi na machicha, amri ya 5, 2°;<br>- Kukata (kuangusha, kuharibu, kuongoa ao kutosha mimea ao miti isiyo pandwa, amri ya 5, 3°;<br>- Kuingiza aina ikiwa gani ya nyama ao ya mimea;<br>- Kutafuta ndani ya udongo, kuchimba mifereji, kuuliza uliza ao kupekuza, kutwa vyombo na kufanya kazi ya aina zote zenye zina weza kubadirisha hali ya udongo ao ya pori, amri ya 5, 5°;<br>- Kufunga mito, kuondoa ao kuharibu mara moja ao kwa njia zingine maji, amri ya 5, | - Ndani ya matimizi ya mapashwa zao wafanya kazi wanaweza zuunguka, ma waziri wa ibada, wa ganga ao wanao saidia waganga wanao itwa kwa upesi kwa ajili ya wagonjwa na wakaaji wa udongo unao patikana ndani ya akiba, amri ya 4, sehemu ya 2;<br>- Kwa hali ya matembezi, kuzunguuka na kulala (kupanga), amri ya 6;<br>- Kujilinda (kupigana) kwa sheria, amri ya 5;<br>- Kwa mafunzo ya tabia ya wa nyama,ina wezekana kusogea, kuuzi (kusumbua) kufunga picha na kukamat wanyama, amri ya 7, 3°;<br>- Kwa shabaa ya kuchunga akiba ya aina za nyama ao mimea, ina wezekana kuepusha kuzaana kwa zaidi ya wa moja ao kutenda namna zingine;<br>- Kwa ajili ya kazi ya mafunzo ya utalaamu, amri ya 7, 1°; |

| | |
|---|---|
| 6°;<br>- Kufanya yote inayo fanana uvuvi, amri ya 5, 7°;<br>- Kurusha ndege ya anga kwa urefu wa anga chini ya mita 300. | - Sheria za waziri zinazo ruhusia wakaaji kuvua samaki ndani ya mito zi moja.<br>Inaonekana ndani ya kibao 3, C, 2. |

### *III.2. Kibao 2 Akiba Ya Mawindo: Sheria 82-002 Ya Mei 22 1982*

| KAZI ZINAZO KATAZWA | RUHUSA KWA YALIYO KATAZWA |
|---|---|
| - Kuingiza ndani ya Jamhuri ya Kidemocrasia ya Kongo nyama za mwitu za kigeni kufuatana na nyama ya taifa yetu, amri ya 3;<br>- Kuingiza nyama za ufugo zinayo ishi pembeni ya watu ao, silaha za moto, mitego ao chombo chochote cha mawindo, kupatikanamo na silaha, kubeba nyama za mwitu zinazo maisha, ngozi zao ao pembe, nyama zao ao mazao zingine zote, amri ya 13, 1°;<br>- Kufuata, kuwinda, kukamata (kunasa), kuogopesha ao kuchafua (kusumbua) aina yote ya nyama ya mwitu hata nyama inayo julikana kuwa za hatari, amri ya 13, 2°; → | - Isipokuwa kwa kupigana vita ya kujiponya ao ya kutokujua namna ingine ya kufanya, amri ya 13, 2 na kumaliza ; |
| - Kuharibisha kwa namna isiyo ruhusiwa makao ya nyama ya mwitu, amri ya 13, 3°;<br>- Kurusha ndege ya anga kwa urefu wa anga chini ya meta 500;<br>- Kuhamisha vijiji vipatikanamo wakati wa muundo wa akiba, amri ya 14, a; → | - Isipokuwa:<br>1° Wakati unaomba kutengeneza |

| | |
|---|---|
| - Kuhamisha wakaaji na muundo wa vijiji vipya ndani ya akiba, amri ya 14, b;<br><br>- Kukata majani yalio pandwa kwa udongo na kwa namna yote, kufanya kazi yenye haina hasara (hatari) ya kuharibu kimia, ustawishi ao kwa matumizi ya nyama, amri ya 14, c;<br><br>- Kuuwa, kunasa (kukamata), kuwinda, kufuata, kusumbua kwa mapenzi binafsi ao kukimbiza kwa njia (kwa namna) yote kwa shabaa ya kuhatarisha wanyama wanao hesabiwa kwa kibao I, amri ya 27; → | makao ya nyama ya mwitu, amri ya 15;<br>2° Wakati unaomba kurahihisha matumizi ya nyama hizo, amri ya 15.<br><br>- Isipo kuwa kwa njia ya ruhusa ya utaalamu, amri ya 27 |
| - Kuondoa ao kuharibu mayayi, machicha yenye kuwekewa ndani ya vyombo vya kukomaza ao ndani ya chicha, amri ya 32; → | - Isipo kuwa kwa lazima ya majifunzo ya utaalamu, amri ya 32; |
| - Kuwinda njiani muhuri, kwa njia ya mashua ya nchi kavu na ambatano yake, viwanja vya ndege na pembeni ya miji mikuu, amri ya 16 ; →<br><br>- Ndani ya ngambo moja ya akiba ya nyama, kuwinda na vyombo na mafanyizio yalio hesabiwa, amri ya 12 kuanzia 1 mpaka 9. | - Isipokuwa:<br>1° Kwa mawindo yaliopangwa kwa shabaa ya kupiganisha, kutawanisha kwa magonjwa moja ya wanyama yanayo hatarisha watu, amri ya 22;<br>2° Kwa sababu ya utaalamu, amri ya 20. |

### *III.3. Kibao 3 : Haki Na Sharti Ya Serikali Na Ya Wakaaji Mbele Ya Matumizi Ya Eneo Ya Kukingwa*

| **III.3.1. Serikali (mwenye) amri ya manufaa-eneo la kukingwa** | |
|---|---|
| **HAKI** | **SHARTI** |
| | |

<table>
<tr><th colspan="2">SHERIA YA MSITU</th></tr>
<tr><td>- Mwenye msitu, amri ya 7, sehemu ya 2 na 3;<br>- Kuzuia na kupiganisha moto wa msitu na wa majani, amri ya 56;<br>- Kuhakikisha, kurudishwa kwa msitu kwa njia ya utungo na matumikisho ya mipango ya kurudishwa upya maumbile na ya kupanda miti, amri ya 77 na 78.</td><td>- Kutunga siasa ya pori ya taifa, amri ya 4 mpaka 6;<br>- Kuweka msitu wa kupangwa unao weza kuwa na upana ukiwa kidogo 15% ya nchi, amri ya 14;<br>- Kushimika mpango wa ujenzi ndani ya kila msitu wa kupangwa, amri ya 17;<br>- Kupana (bei) kwa msitu wa kupangwa kufuatana na ilio andikwa ndani ya cheti cha kupangwa na mipangilio ya mpango wa ujenji, amri ya 18;<br>- Kwa inayo angalia kupangwa kwa msitu, kuachia wakaaji jirani eneo kwa ajili ya kujibia kwa lazima zao za nyumba sawa vile kwa mazao ya msitu na kwa udongo wa kilimo wa muda, amri ya 16, sehemu ya 2;<br>- Kufata wazo linalo faa ya shauri la ujuvi wa jimbo kwa kupanga msitu fulani, amri ya 15;<br>- Kupata wazo linalo faa na wa shauri la ujuvi wa taifa na ya majimbo yanayo husika na msitu kwa kupanga kuliko kwa kipande ao kwa msitu wote;<br>- Kuhakikisha matumizi ya sheria na kanuni inayo ongoza matumikishi daima ya manufaa na kukesha kwa matumizi ya matumikisho ya sasa. Kuona adhabu ndani ya nyaraka;<br>- Sharti la serikali ya kuchunga akiba ya yote inayo angalia maisha mbalimbali ndani ya aina tatu ya msitu.</td></tr>
<tr><th colspan="2">SHERIA 08-08 YA APRILI 8 2008 INAYO SIMAMISHA MWENENDO WA KUPANGA</th></tr>
<tr><td>- Kuweka haki ya kutumia inayo weza fanyika kwa msitu, chumba kinacho husika na matumikishi yake namna ya</td><td>- Kujuvia watu wote na wakaaji jirani ya msitu, amri ya 5 mpaka cha 10;<br>- Kupata wazo la shauri ya ujuvi la jimbo linalo husika na msitu, amri ya 11 na 12.</td></tr>
</table>

| | |
|---|---|
| matumizi ya manufaa, amri ya 13. | |
| **SHERIA 75-024 YA JULAI 22 1975 JUU YA KUUNDWA KWA SEHEMU YA KULINDA** | |
| - Kuunda sehemu (SECTEURS) ya kulinda, amri ya 1. | Kulipa wakaaji mbele ya yote ikiwa watahamishwa, amri ya 4; |
| **SHERIA YA RAISI 69-041 YA AGOSTI 22 JUU YA KUCHUNGA AKIBA YA UMBO** | |
| - Kuunda akiba nzima, amri ya 1. | Kulipa malipo yanayo faa kwa wenye kutoshwa, amri ya e, sehemu ya 2. |

### III.3.2. Chumba cha Kongo juu ya kuchunga akiba ya umbo ao watumishi wengine

| HAKI | SHARTI |
|---|---|
| - Inatoa malipo (AMENDES) na kunyanganywa kunako semwa kwa njia ya sheria ya Raisi, amri ya 12-sheria ya 63-041 ya Agosti 22 1969;<br>- Mazao ya matumikisho, kipengele cha 6-sheria ya Aprili 10 2010;<br>- Malipo nyingine inayo angalia kodi inayo wezekana, amri ya 6-sheria ya 10 Aprili 10 2010. | - Ujenzi wa mitaa aliyo pewa kufuatana na sheria ya sasa;<br>- Kukusanya kodi, malipo zingine zilizo angalia kodi yenyewe anapashwa kulipa na kuletwa mfuko wa muhuri akiba ya taifa ao kwa yeyote anaye mamlaka, amri ya 4-sheria ya Aprili 10 2010. |

### III.3.3. Wakaaji na vikundi vya wakaaji wa nafasi

| HAKI | SHARTI |
|---|---|
| ***III.3.3.1. Pori za kupangwa*** | |
| **SHERIA YA MSITU** | |
| - Kujuviwa mbele ya kupangwa kwa msitu, amri ya 15;<br>- Kuwa wenye kufaidika na haki ya kutumia zinazo hesabiwa ndani ya amri ya 39. | - Kuheshimu haki ya kutumia inayo wekwa ndani ya kila aina ya msitu, amri ya 36; |

| | |
|---|---|
| | - Kuto kulima ao kutumika kazi zingine zinazo haribu ujenzi daima wa msitu wa kupangwa, amri ya 39. |
| **SHERIA YA WAZIRI YA 08 YA APRILI 8 2008 INAYO WEKA MWENENDO WA KUPANGA ULIO PANGWA KUTIA PEMBENI MSITU** | |
| - Kujuviwa mbele, amri ya 5 mpaka 7;<br>- Kuthamini umbo na upana wa haki ya kuwalipa, amri ya 8 mpaka 10;<br>- Kuitika mambo haya, amri ya 10;<br>- Kuwa na namna ya kuuliza kama mambo haya timiliki vizuri, amri ya 10. | |
| ***III.3.3.2. Akiba maumbile nzima*** | |
| • AKIBA YA TAIFA JUU YA UFUGO YA VIRUNGA, A.R. 4 MAI 1937<br>- Haki ya wakaaji wa asili ya kunywisha nyama zao maji ndani ya visiwa safi ya GIHORWE;<br>- Haki ya wakaaji wa asili ya kuvua samaki ndani ya mto RUTSHURU; mipaka;<br>- Haki ya wakaaji wa asili ya kuwinda ndani ya eneo tatu ilio katwa mipaka;<br>- Haki ya wakaaji wa asili ya kuvuna junvi juu ya kilima kinacho toa moto Rumoka, ya kokwa pembeni ya ngambo ya kuume ya mto Semliki, ya kukata miti (mbao) ya majengo juu ya mlima Buhuku;<br>- Haki ya kuchuma na kukata kuni;<br>- Haki ya kuzunguuka bila kutiliwa mpaka hata moja kwa njia tatu munamo tembeleo gari: ya Goma, Rutshuru, Kigota, Kabasha-Humu, Goma-Sake, pembeni ya kijito ya Kivu.<br>• AKIBA YA TAIFA JUU YA UFUGO WA GARAMBA, D. 17/03/1938<br>- Haki ya wakaaji wa asili wa kuvua samaki ndani ya nafasi (bief) yaliyotiwa mipaka kwenye amri ya 2, nucta 1 ya sheria ya Waziri; | Kuheshimu yote yaliyo katazwa ya vitendo vilio wekwa na sheria ya Raisi ya Agosti 22 1969 juu ya kuchunga akiba ya umbo pia sehria ya Mei 28 1982 juu ya kanuni ya mawindo. |

| | |
|---|---|
| • AKIBA YA TAIFA YA JUU YA UFUGO YA UPEMBA, D./15 Mei 1939<br>- Haki za wakaaji wa asili ya kuvua samaki ndani ya kipande kimoja cha (bief) ya Lufira;<br>- Kiwanda cha kutoa chunvi cha lukoka. | |
| ***III.3.3.3. Yote yanayo angalia mawindo*** | |
| - Yote yanayo angalia mawindo ina chungwa akiba katika mtaa wa Faradje, Ar. 00007 ya Februari 14 1974;<br>- Yote yanayo angalia mawindo inayo chungwa akiba katika mtaa wa Dungu, Ar. wa Februari 14 1974;<br>- Yote yanayo angalia mawindo inayo chungwa akiba ndani ya mtaa wa Faradje, ya Watsa na Dungu, Ar. 0002 ya Februari 14 1974;<br>- Yote yanayo angalia mawindo inayo chungwa akiba ndani ya mtaa wa Bondo, Ango na Dungu, Ar. 00023 ya Februari 14 1974;<br>- Yote yanayo angalia mawindo inayo chungwa akiba ndani ya mtaa wa Rutshuru, Ar. 00024 ya Februari 14 1974;<br>- Wakaaji wa vijiji vinavyo patikana ndani ya akiba ya mawindo wanachunga haki zao ya asili juu ya mawindo kwa ajili ya lazima yao moja ya malisho;<br>o Wanapashwa kupata hata hivyo kibaruwa kinacho ruhusu kwa kila mtu binafsi anae pangwa na mwenye madaraka juu ya msitu wa akiba na watawinda nyama tu zenyi hazikingwe na wata ziwinda kwa msaada wa mawindo ya asili yanayo ruhusiwa wasipo tumia bunduki ya PISTON ao ya SILEX, amri ya 12. | |

## IV. KWA KIFUPI

Muundo wa akiba maumbile nzima wa hifadhi ya taifa juu ya ufugo na za sehemu ya kulinda yapo chini ya uwezo wa Raisi. Ni Waziri anae husika na mawindo ndie anatia, kupitia shauri ya mawaziri, na kufuatana na ombi la liwali wa jimbo, sehemu moja ya kata inayo chungwa akiba ya nyama ao ya yote inayo angalia mawindo.

Maazitu ya kazi zilizo changa vikundi vya ma jimbo mbalimbali juu ya ukaguzi wa sheria 69-041 ya Agosti 22 1969, ili chumba cha Kongo kinacho husika na kuchunga akiba ya umbo kiweze kuanzisha matumikisho yanayo ombwa kwa ajili ya akiba maumbile ya akiba ya nyama na ya yote inayo angalia mawindo, inafaa kumpa manufaa ya watu na pesa inayo faa. Kwa hiyo, haifai kukana nafasi muhimu ya serikali ndani ya matumikishi na ya kuleta pesa juu ya kazi ya eneo hizi ; kwani ni ujumbe wa mafaa ya watu wote wenyi bei ya ushirika, uchumi na mafunzo ya maisha ni kali saana.

Kwa inayo angalia msitu wa kupangwa, zinaundwa na Waziri anae husika na msitu kwa njia ya sheria ya Waziri. Sheria hii ina weka aina ya kila msitu, jina lake, namna ya matumikishi ya manufaa yake yenyi inakatazwa juu yake, haki ya kutumikia yenye inaweza timizwa humo na chumba kinacho husika na matumikishi yake.

Kupanwa kwa bei kwa msitu wa kupangwa inafanyika kufuatana na inayo andikwa ndani ya cheti cha kupangwa na mipangilio ya mpango wa ujenzi kama vile inayo semwa ndani ya sheria ya Waziri. Inafaa kutayarisha yote yanayo faa ili chumba kinacho tajwa hapa juu kitimize kazi yake vizuri.

# V. VITABU VILIVYO TUMIWA

## *V.I. Nyaraka Za Serikali (Zinazo Julikana)*

- Sheria ya Waziri ya Novemba 26 1934 inayo unda chumba cha hifadhi ya taifa juu ya ufugo;
- Sheria ya Raisi 69-041 ya Agosti 22 1969 juu ya kuchunga akiba ya umbo;
- Sheria 71-008 ya Desemba 31 1973 juu ya utawala ya vitu, kanuni ya udongo na vitu vyenyi haviwezi hamishwa na kanuni ya uhakiki;
- Sheria 75-023 ya Julai 22 1975 juu ya muundo wa chumba cha Kongo juu ya kuchunga akiba ya umbo, kwa kifupi, «ICCN»;
- Sheria 75-024 ya Julai 22 1975 juu ya muundo wa sehemu ya kulinda;
- Sheria ya Raisi 75-231 ya Julai 22 1975 inayo weka kazi ya offisi ya manzingira, uchunguzi wa akiba ya umbo na matembezi;
- Sheria ya Raisi 78-190 ya Mei 5 1978 juu ya (KATIBA) ya chumba cha Jamhuri kinacho itwa chumba cha Zaïre juu ya kuchunga akiba ya umbo kwa kifupi «IZCN»;
- Sheria 81-013 ya Aprili 1 1981 juu ya sheria yote inayo angalia madini na mafuta;
- Sheria 82-002 ya Mei 28 1982 juu ya kanuni ya mawindo;
- Sheria ya Waziri 081 ya Julai 2 1998 juu ya mwenendo wa inchi na uhakimu wa Jamhuri ya Kidemocratia ya Kongo;
- Sheria 007-2002 ya Julai 11 2002 juu ya sheria ya madini;
- Sheria 011-2001 ya Agosti 29 2002 juu ya sheria ya msitu;
- Katiba ya Jamhuri ya Kidemocratia ya Kongo ya Februari 18 2006;
- Sheria ya Raisi 07-081 ya Mei 16 2007 inayo pana kazi za offisi za wizara;
- Sheria ya Waziri 08-08 ya Aprili 8 2008 inayo tiya mwenendo wa kupangwa na kuondoshwa kwa msitu;
- Sheria no 009/002 ya Mei 7 2009 juu ya kutia mipaka ya eneo ya maji ya Jamhuri ya Kidemocratia ya Kongo;
- Sheria ya Waziri 10-15 ya Aprili 10 2010 inayo weka katiba ya chumba cha Jamhuri kinacho itwa chumba cha Kongo juu ya kuchunga akiba umbo.

## *V.2. Mapatano Ya Mataifa*

- Mapatano yanayo angalia kuchunga akiba ya nyama na ya majani kwa hali ya kuumbwa mwitu ya Novemba 8 1933;

- Mapatano yanayo angalia ndege wa anga wa mataifa ya Decemba 7 1944;
- Mapatano ya Africa juu ya kuchunga akiba ya umbo na ya manufaa maumbile ya Septemba 15 1968;
- Mapatano yanayo angalia eneo ya baridi inayo kuwa ya faida kwa mataifa, kwa upekee kama makao ya nyama ya mwitu ya Februari 2 1971;
- Mapatano yanayo angalia ukingo wa mali ya dunia ya asili na maumbile ya Novemba 22 1972;
- Mapatano juu ya uchuluzi wa mataifa ya aina ya nyama na ya majani ya mwitu inayo hatari ya kumalizika ya Machi 3 1973;
- Mapatano juu ya umbali mbali wa maisha ya Julai 5 1972.

### *V.3. Vitabu Ao Maandiko Mbalimbali*


Doumbé-Billlé (St.)

Droit international des aires protégées, in Les aires protégées en droit comparé, Actes des 2èmes journées du DEA – Etudes Environnement, Tunis, 2001, pp. 12-21.

Durieux (A.)

L'Institut des Parcs Nationaux du Kongo Belge, Les Novelles – Droit colonial, Tome IV, Bruxelles, Larcier, 1948, pp. 567-599.

Du Saussay (Chr.)

Statuts fonciers et politique forestière, Etude législative, n°41, Rome, FAO, 1986, 59p.

FAO

Thésaurus multilingue du foncier, version française, Rome, FAO, 1999, 216 p.

Du Saussay (Chr.) et Wilkison (P.)

La conservation de la nature au Zaïre – Ecologie et législation – Rapport préliminaire, FAO-TCP/ZAI/6651, S.D., 117 p.

Lubini Ayingweu et Ohoto Amana L.B.

La réserve de la biosphère de Luki (Bas-Zaïre), in Actes du séminaire – Environnement et Développement durable, Brazzaville, 1988, pp. 109-114.

Maldague (M.)

Le processus de la planification appliquée à la gestion des ressources naturelles, in Actes du Séminaire –Environnement et Développement durable, Brazzaville, 1989, pp. 83-104.

Matuka Kabala

Des outils de gestion pour l'environnement de l'an 2000 –Le rôle de l'Unesco – Réserves de la biosphère et patrimoine mondial, in Actes du Séminaire – Environnement et Développement durable, Brazzaville, 1989, pp. 59-73.

Ministères de l'Environnement, Conservation de la Nature et Tourisme

Plan National d'Action Environnemental (PNAE), Etat actuel de l'environnement au zaïre, Septembre 1996, 247 p., plus annexes législation environnementale et cadre institutionnel de l'environnement.

Ministères des Affaires foncières, Environnement, Conservation de la Nature, Pêche et Forêts

Stratégie nationale et Plan d'action de la biodiversité, Kinshasa, 1999, 134p.

Ministères de l'Environnement, Conservation de la Nature et Tourisme

Stratégie nationale de conservation communautaire en République Démocratique du Kongo (2007-2011), Kinshasa, 2008, 37 p.

Mugangu (Tr.)

Types de gouvernance et catégories d'aires protégées suivant la classification de l'UICN, Les catégories de l'UICN (1994), Les modes de gouvernance et les objectifs de gestion, 12 août 2008, 7 p.

Prieur (M.)

Les aires protégées en droit français, in Les Aires protégées en droit comparé, in Actes des 2èmes journées du DEA – Etudes Environnement, Tunis, 2001, pp. 38-50.

Sakata (G.)

Code forestier : Analyse du statut juridique de la forêt et des acteurs de gestion, in «Quel avenir pour les forêts de la République démocratique du Kongo, Tervuren, Reflexion and discussion paper 2007 :01, pp. 30-33.

Sakata (G.)

Le code forestier et le code minier de la RDC : Rôle des acteurs et impact socio-économique, Essai comparatif, Rapport, Tervuren, Musée Royal de l'Afrique Centrale, 2007, 40 p.

Sakata M. Tawab (G.)

Code forestier et ses mesures d'application – Commentaire pratique, Louvain-la-Neuve, Bruylant-Académia, 2010, 270 p.

Staner (P.)

La chasse et la pêche au Kongo belge et Ruanda-Urundi, Les Novelles – Droit colonial, Tome IV, Bruxelles, Larcier, 1948, pp. 545-565.

Vundu dia Massamba (V.) et Kalambay Lumpungu (G.)

Le code forestier commenté et annoté – Loi n°11-2002 du 29 août 2002, Kinshasa, 2009, 109 p.

**Traduction réalisée par l’ONGD «EDEN»**